ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake

18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo

43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali	-	Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf	-	Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	-	Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa	-	Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa	-	Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	-	Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini	-	Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy	-	Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali	-	Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Thelathini na Nne - Tarehe 23 Juni, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Taarifa ya Spika Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba niwasilishe Barazani Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara na Kuweka mambo mengineyo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika: Samahani ni Taarifa ya Spika likuwa ni ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Samahani Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako wakati najibu swali Namba 176 linalohusu juu ya watu wenye mahitaji maalum, niliulizwa swali la nyongeza na Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, Viti Maalum aliyetaka kujua idadi ya wanafunzi waliofaulu katika miaka mitano (5) iliyopita kuanzia 2012 – 2016.

Mhe. Spika, kwanza wanafunzi wenye mahitaji maalum wako wengi ukizingatia na mahitaji yao. Kwa mfano kuna mayatima, wanafunzi wanaoishi kwenye mazingira magumu, wanafunzi wenye maradhi sugu, walemavu wa ngozi (Albino), wenye uzito wa kujifunza, wenye ufahamu mkubwa, walemavu wa kusikia (viziwi), walemavu wa macho (wasioona), walemavu wa viungo na kadhalika. Lakini kwa upande wa mitihani uchambuzi wa wanafunzi wenye ulemavu waliofaulu katika viwango mbali mbali wakiwemo Albino, Wasioona na Viziwi tutabainisha.

Vile vile wanafunzi waliokwenda Michipuo, Kidato cha Tatu, Kidato cha Tano na Waliokwenda Vyuo Vikuu kuanzia mwaka 2012 hadi 2016 wakiwemo wanawake 27 na wanaume 22 ambao jumla yao ni wanafunzi 49. Wanafunzi hao ni kama ifuatavyo:-

ORODHA YA WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUM WALIOFAULU KUANZIA 2012 - 2016

NAMBA	MWAKA	AINA YA ULEMAVU	DARASA ALILOINGIA	JINSIA	SKULI ALIYOKWENDA
1	2014	ASIYEONA	KIDATO CHA TATU	M'MKE	MADUNGU SEKONDARI
2	2014	KIZIWI	KIDATO CHA TATU	M'ME	MAKOONGWE SEKONDARI
3	2014	ASIYEONA	KIDATO CHA TATU	M'ME	MADUNGU SEKONDARI
4	2014	ASIYEONA	KIDATO CHA TATU	M'ME	VIKOKOTONI SEKONDARI
5	2014	ASIYEONA	KIDATO CHA TATU	M'ME	SKULI YA PAJE
6	2014	KIZIWI	KIDATO CHA TATU	M'ME	M'KWEREKWE "A" SEKONDARI
7	2014	ASIYEONA	KIDATO CHA TATU	M'ME	HAILE SELLASSIE
8	2014	ASIYEONA	KIDATO CHA TATU	M'ME	HAILE SELLASSIE
9	2014	ASIYEONA	KIDATO CHA TATU	M'KE	HAILE SELLASSIE
10	2014	KIZIWI	KIDATO CHA TATU	M'ME	SHAMIANI
11	2015	ASIYEONA	KIDATO CHA TATU	M'KE	BWEFUM
12	2015	ASIYEONA	KIDATO CHA TATU	M'KE	HAILE SELLASSIE
13	2015	KIZIWI	KIDATO CHA TATU	M'KE	M'KWEREKWE "C" SEKONDARI
14	2015	KIZIWI	KIDATO CHA TATU	M'KE	M'KWEREKWE "C" SEKONDARI
15	2015	KIZIWI	KIDATO CHA TATU	M'KE	M'KWE "C" SEKONDARI
16	2015	KIZIWI	KIDATO CHA TATU	M'KE	M'KWEREKWE "A" SEKONDARI
17	2015	KIZIWI	KIDATO CHA TATU	M'KE	SKULI YA MAKUNDUCHI
18	2015	KIZIWI	KIDATO CHA TATU	M'ME	SKULI YA KINYASINI
19	2015	ALBINO	KIDATO CHA TATU	MKE	HAILE SELLASSIE

20	2015	KIZIWI	KIDATO CHA TATU	MKE	JANG'OMBE SEKONDARI
21	2015	ALBINO	MICHEPUO	M'ME	SEKONDARI J K U
22	2015	ALBINO	MICHEPUO	M'ME	SKULI TUMEKUJA
23	2016	KIZIWI	KIDATO CHA KWANZA	M'MKE	MIKINDANI
24	2016	KIZIWI	KIDATO CHA PILI	M'MKE	M'KWEREKWE "A" SEKONDARI
25	2016	ASIYEONA	KIDATO CHA TATU	M'MKE	PONDEANI
26	2016	ASIYEONA	KIDATO CHA TATU	M'ME	MCHANGA MDOGO
27	2016	ASIYEONA	KIDATO CHA TANO	M'KE	SHAMIANI/ HAKURIPOTI
28	2016	KIZIWI	MICHIPUO	MME	CHASASA
29	2016	ASIYEONA	KIDATO CHA TANO	MME	FARAJA
30	2012	ASIYEONA	MICHEPUO	M'ME	VIKOKOTONI SEKONDARI
31	2012	ASIYEONA	MICHEPUO	M'MKE	VIKOKOTONI SEKONDARI
32	2012	KIZIWI	KIDATO CHA TATU	M'ME	M'KWEREKWE "A" SEKONDARI
33	2012	KIZIWI	KIDATO CHA TATU	M'MKE	M'KWEREKWE "A" SEKONDARI
34	2013	ASIYEONA	KIDATO CHA TATU	M'ME	HAILE SELLASSIE
35	2013	KIZIWI	KIDATO CHA TATU	M'MKE	M'KWEREKWE "B" SECONDARI
36	2013	KIZIWI	KIDATO CHA TATU	M'ME	UTAANI "B"
37	2012	ASIYEONA	DIGRII SHERIA	M'MKE	ZANZIBAR UNIVERSITY
38	2013	ASIYEONA	DIGRII UALIMU	M'ME	UNIVERSITY DODOMA
39	2014	ASIYEONA	DIPLOMA YA UTAWALA	M'MKE	SUZA
40	2014	ASIYEONA	DIPLOMA YA UALIMU	M'ME	SUZA
41	2014	KIZIWI	DIGRII YA UUGUZI	M'ME	ZANZIBAR UNIVERSITY
42	2014	KIZIWI	DIGRII YA AFYA	M'ME	SUZA

43	2015	KIZIWI	DIGRII YA UTALII	M'MKE	SUZA
44	2015	KIZIWI	DIGRII UALIMU	M'ME	ZANZIBAR UNIVERSITY
45	2016	ASIYEONA	DIPLOMA YA UALIMUMAANDALIZI	M'MKE	SUZA
46	2016	ASIYEONA	DIPLOMA YA UALIMUMAANDALIZI	M'MKE	SUZA
47	2016	KIZIWI	DIPLOMA YA ELIMU MJUMUISHO	M'MKE	SUZA
48	2016	KIZIWI	DIPLOMA YA ELIMU MJUMUISHO	M'MKE	SUZA
49	2016	ALBINO	DIGRII YA UALIMU	M'MKE	AL-SUMEIT/ CHUKWANI

Mhe. Spika, nakushukuru sana ahsante.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Waheshimiwa Wajumbe napenda pia nichukue nafasi hii kutaka kutoa taarifa katika Mkutano huu wa Sita wa Baraza la Sita la Wawakilishi unaoendelea, Baraza hili lilipitisha Miswada mitano ya Sheria, miongoni mwa miswada hiyo ni Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar Nam. 4 ya Mwaka 2015, kama inavyotakiwa chini ya Kanuni ya 91(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2016, naomba kutoa taarifa kwamba, Mswada huo sasa umekuwa sheria kamili baada ya kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Ripoti ya Utekelezaji ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar, kuhusu utekelezaji wa Oktoba, 2013 hadi Disemba 2016.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 3 ya mwaka 1985 na kuanzishwa upya Mahakama ya Kadhi na kuweka masharti mengine yanayohusiana nayo kusomwa kwa mara ya kwanza.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara na kuweka mambo mengineyo yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Suleiman Makame Ali (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka hati mezani ya maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria, Utawala Bora na Idara Maalumu kuhusu Ripoti ya

Utekelezaj na Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar kuhusu utekelezaji wa kipindi cha Oktoba, 2013 hadi Disemba 2016.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI

Nam 159

Uhaba wa Tenki la Kuwekea Mafuta kwa Upande wa Pemba

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:

Mhe. Spika, awali ya yote nami niungane nanyi tumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema mwenye Kurehemu, aliyeumba Mbingu na Ardhi na vilivyomo vyote na tumatakie kheri Mtume wetu Muhammad *(S.A.W)* na Ramadhani hii. Mhe. Spika, naomba kujibiwa swali langu Nam. 159.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inajitahidi sana katika kuleta maendeleo ya Zanzibar na wananchi wake, lakini katika kisiwa cha Pemba suala la Tenki la Mafuta bado ni changamoto kwani pamoja na kuwa shida ya mafuta lakini lipo tenki moja tu la kuweka mafuta, suala hili naliona sio busara sana.

(a) Je, serikali ina mpango gani kuongeza matenki ya kuweka mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa.

(b) Kama mpango upo ni lini suala hili litatekelezwa na kama halipo serikali inalionaje suala hili.

(c) Je, yapo maeneo yaliyotengwa kwa shughuli ya kuweka mafuta Pemba na kama hayapo serikali haioni umuhimu huo kabla serikali haijaingia migogoro na wananchi kwa ajili ya maeneo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 159 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, serikali kupitia wizara yangu imeona ipo haja ya kujenga matangi mapya ya ziada ili kukidhi ongezeko la mahitaji ya mafuta.

(b) Mhe. Spika, utekelezaji wa mpango huu unaweza kufanywa na serikali kwa kupitia taasisi yake ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (*ZURA*), ambayo moja kati ya mipango yake ni kuwekeza katika kuwepo kwa akiba ya kutosha ya mafuta nchini na pia kwa kuwashirikisha wananchi na wawekezaji ambao watataka kuwekeza katika suala hili la ujenzi wa matangi ya kuhifadhia

mafuta. Yupo mwekezaji ambaye tayari ameonyesha nia ya kutaka kuwekeza katika jambo hili Kisiwani Pemba na amekuwa akifanya utafiti wa kina juu ya eneo lipi linaweza kumridhi katika kujenga matangi hayo pamoja na mazingira mazuri ya kina cha maji kwa meli itakayoleta shehena kubwa ya mafuta.

(c) Mhe. Spika, Zanzibar ni nchi ya visiwa na hivyo uletwaji wa mafuta nchini utatumia njia ya bahari. Mpango wa serikali ni kutumia maeneo ya bandari ya bahari iliyopo karibu na Wesha kwa ujenzi wa miundombinu ya mafuta inayojumuisha matangi ya kuhifadhia mafuta pamoja na bahari ya kushushia mafuta hayo. Maeneo yote ya bandari ni mali ya serikali na yamewekewa mipaka iliyopimwa. Serikali haitarajii kuingia katika migogoro na wananchi katika utekelezaji wa shughuli hii. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, na mimi nimpe pongezi sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina swali (a) na (b) la nyongeza. Kwa kuwa matangi yale ni kama yalivyopangwa ni petroli, dizeli na mafuta ya taa ni matatu tu, kwa kuwa kuna haja kubwa kwa kutokana na maendeleo makubwa Pemba, vifaa hivyo vinatakiwa au nishati hiyo inatakiwa sana. Lakini hakuna hata *reserve* moja ya *tank* ambalo linaweza kuwa kama itatokea dharura likaweza kuchukua nafasi ile. Nimuulize Mhe. Naibu Waziri kwamba:

(a) Je, ana mpango wa kuongeza angalau *tank* moja katika eneo lile ambalo kwa sasa hivi ndio linafanya kazi ili liwe *reserve* ya kutokea dharura kutokana na hali halisi.

(b) Katika mpango mkubwa ni maeneo gani ambayo amejipanga kwa ajili ya kutafuta eneo jipya la kisasa linaloendana na matakwa ya maendeleo au kasi ya nishati hiyo huko Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo. Kwanza naomba nimueleweshe kwamba ma-*tank* ambayo yapo kwa sasa Wesha ni matano ambayo yanatosha kwa kiwango cha sasa kutokana na mahitaji halisi ya watumiaji wa mafuta Kisiwani Pemba. Kwani wanatumia wastani wa 1,650,000 na ma-*tank* yaliyoko sasa yana uwezo zaidi ya lita 2,000,046.

Hata hivyo, swali la (b) kama nilivyokuwa nimesema yupo mwekezaji ambaye kaonesha nia ya kuwekeza pale na anafanya utafiti. Kwa hiyo, tusubiri utafiti wa kina ambao anaendelea nao utatuonesha wapi na wingi gani yawekwe. Ahsante sana.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b). Kwanza nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo yanaonesha azma njema ya ujenzi wa *deport* mbali mbali lakini kushirikiana na wawekezaji wazalendo. Lakini katika hatua hiyo hiyo ya msingi kabisa kuna kampuni ya *Zenji Petrol Guides*, ambayo ina asili ya Vituo vya Mafuta kama hivyo masuala ya ujenzi wa *deport*. Katika eneo la Mtoni waliomba vibali na wamepatiwa

process zote zikakamilika mpaka ripoti za kimazingira, lakini hatimaye wizara yake ikamzuwia. Sasa katika hatua ya utekelezaji wa kudai haki alikwenda Mahakamani na Mahakama ikatoa hukumu kuwa ana haki ya kuendelea na ule mradi, lakini pia serikali ikatakiwa ilipe fidia ya ile kesi.

(a) Je, wizara yake inajua hatua hii ya ulipaji wa gharama hizi baada ya kwisha kwa kesi.

(b) Kama inaelewa ni kiasi gani ni lini watazilipa fedha hizi kwa mujibu wa utaratibu ili mwekezaji yule aendelee na ujenzi wake. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Kwanza wizara yangu haijapokea bado *order* ya Mahkama, lakini la pili naomba niseme kwamba Mhe. Jaku Hashim maana yake lazima a-*declare interest*, Mhe. Jaku ameniona na ameniambia hili...

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mimi siye niliyeuliza swali siwezi ku-*declare interest* aniombe radhi Mhe. Waziri swali halikunihusu mimi.

Mhe. Spika: Samahani subiri kwanza, naomba ukae kwanza Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba tena kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa swali lake kwamba, wizara yangu bado hatujapokea *order* ya Mahkama, lakini naomba niseme kwamba Mhe. Jaku Hashim ameniona katika hili na ameniambia kwamba hii kesi kama ilivyoelezwa na Mhe. Miraji Khamis, nikamwambia nimekusikia lakini serikali hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria na utaratibu na tutalifanyia kazi pale ambapo tutapolipokea, kwa hiyo nitakujibu. Hivyo naomba niseme hili na naomba niseme wazi kwa sababu nimelipokea kutoka kwake kwa hiyo lilivyokuja sijalipokea rasmi kutoka serikalini. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, nishukuru sana kwamba mimi siye niliyeuliza swali.

Mhe. Spika: Sikupi nafasi ya kuuliza swali la nyongeza nakupa...

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, hoja yangu tuna kanuni hizi tumepewa suala kama linanihusu mimi ndio ninge-*declare interest* aulizwe Mhe. Suleiman Sarahan Said nilimwendea mimi nikamwambia hili swali ikawa tumelipanga mimi na yeye na huu Mwezi wa Ramadhani? Kwa hiyo, Waheshimiwa Mawaziri wanapokuja huu muongozo waufuate.

Mhe. Spika: Mheshimiwa hukumfahamu waziri, waziri alichosema wewe na yeye mlishawahi kuzungumza suala hili, umeshawahi kumpelekea jambo hili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, mwanzo alisema ni-*declare interest* nilisikia masikio yangu sawa.

Mhe. Spika: Hapana, mimi nasikiliza huku Mheshimiwa, ni kwamba hili jambo uliwahi kuzungumza naye waziri yaani mimi sioni tatizo. Ahsante sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini pili niseme tu kwamba niseme tu kwamba Serikali yetu ya Zanzibar na Serikali ya Muungano inatoa hamasa kubwa sana kwa wananchi wake kuekeza katika nchi na kwa bahati nzuri tunaelewa tu kwamba kuna makampuni mbali mbali ambayo yamejitokeza kuekeza katika sehemu hii ya mafuta, kutafuta maeneo mbali mbali kujenga ili kuongeza uwezo wa kukusanya mafuta ambayo ni rasilimali muhimu sana kwa nchi.

Je, kwa kuwa mwananchi huyo fulani ambaye simjui amejitokeza na yuko tayari kwa haraka kuekeza hiyo rasimali mafuta, wazara pamoja na makubaliano ambayo siyalewi wana mapango gani wa kumpatia urahisi wa kuendesha biashara hiyo ili kuongeza maisha na pato ya nchi katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa naiba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji,Nishati na Mazingira naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Serikali haina tatizo na mwekezaji yoyote yule ili mradi tu utaratibu na sheria zifuatwe. Ahsante sana.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mheshimiwa nasimama kanuni ya 63, 7 sijui utaniruhusu niisome au itatosheleza.

Mhe. Spika: Endelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: 63 Mhe. Spika, kuhusu utaratibu baada ya 63 inakuja 67 Spika atawajibika kutilia nguvu kanuni zote za Baraza endapo Mjumbe yoyote hatoridhika na maamuzi ya Spika, na anaweza kuwasilisha baada ya kutoridhika kwake.

Mheshimiwa leo Ijumaa niliahidiwa humu ndani kuhusu kauli yangu niliyoitoa kutaka serikali wala sikutaka kutumia hoja ya dharura. Niliwapa serikali ili wakajipange ili

wananchi waliotutuma wapaate kusikiliza jawabu kutoka kwa serikali ni suala la Mnazi Mmoja kuhusu *lift* na sijapata kauli mpaka muda huu na kitu chenyewe sifikirii kama kina gharama kubwa kama hicho.

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa.

MUONGOZO

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, nimeunuka na kanuni ya 42 kuleta hoja ya dharura, lakini hoja ya dharura hii nilikuwa sitaki Baraza lako liakhirishe kazi zake isipokuwa serikali i-*take note*.

Mhe. Spika, hivi sasa katika Mji wetu wa Zanzibar pamoja na viunga vyake *ATM* za *PBZ* hazifanyi kazi zote na wananchi wetu waumini wa dini ya Kiislamu wanahitaji mahitaji makubwa sana kuna foleni kubwa sana. Sasa ningeomba ilichukuwe ili kwa haraka sana waumini wasipate tabu ya kuhangaika pesa za chakula na mambo mengine za huduma hizi inaleta bughudha kubwa sana kwa wananchi wetu. Mhe. Spika, muongozo wako.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Machano Othman Said.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, na mimi naomba muongozo kwa kifungu 42. Lakini kama Mhe. Mohammed Said tuakhirishe shughuli za Baraza isipokuwa tu tupate maelezo ya serikali.

Serikali imejitahidi sana kujenga barabara nzuri ya Meli mbili mpaka Fuoni na nzuri sana. Lakini pale eneo ambalo palikuwa na maji mengi pale yamejaa Mwanakwerekwe barabara imeharibika na foleni sasa hivi ni kubwa hata ile barabara ya Nyumba mbili nayo imezidiwa. Kwa hivyo, kupitia serikali tutaiomba ifanye matengenezo ya dharura katika eneo lile ili kuondoa tatizo katika hii Sikukuu ya Idd kwa haraka, ingawa katika maeneo mengine ya Mjini wameshaanza kufanya matengenezo basi pale wafanye kwa haraka Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante Waheshimiwa na Mhe. Hassan Khamis Hafidh na wewe una jambo lako pia haya nikusikilize kabisa na wewe.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunifruhusu. Mhe. Spika, nainuka na kanuni ya 63, 42. Mhe. Spika, Jumamosi iliyopita nilitembelea Donge Chechele kunakochimbwa mchanga. Mhe. Spika, baada ya kutembelea huko kuna mambo mengi niliyagundua mengi. Lakini nataka kulieleza moja au mawili ambayo ni muhimu na naomba serikali *take note* ambayo sitaki yajadiliwe.

Mhe. Spika, niligundua kuna *Scavator* SE namba 550 inachota mchanga kutia kwenye gari. Mhe. Spika, inasemekana scavator ni ya mtu imekodiwa laki tisa kwa siku ...

Mhe. Spika: *Exstavator* au

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: *Stavator* kijiko.

Mhe. Spika: *Ni loader*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: *Loader yes,* inasemekana *scavator* hii ni ya mtu imepelekwa imekodiwa laki tisa kwa siku lakini kwa siku ya Ijumaa ilitia magari 356 sawa sawa karibu na milioni 17. Sasa athari yake Mhe. Spika, kabla ya kuwa na *scavator* hii kulikuwa kuna vijana karibu 400 mpaka 500 wanafanya kazi pale na nafasi yao imechukuliwa na wajanja.

Naiomba serikali ifatilie suala hili na iondoshe scavator hii kwa haraka kwa sababu ni ya mtu. Mpaka tunaondoka saa 5:20 katika lile eneo scavator hii ilikuwa imeshatia mchanga gari 176 karibu sawa sawa na milioni 10.

Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa hii naomba serikali ijuwe jambo hili ni la mtu na anafanya ujanja, kwanza wanawadhulumu wale wananchi ambao pale walikuwa wanafanyakazi wamewaondosha. Lakini pili Mhe. Spika, ujanja huu unafanyiwa serikali si kitu sahihi hata kidogo. Tunaiomba *scavator* hii iondoke kwa haraka na wananchi wale waendelee kufanya kazi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kuhusu utaratibu.

Mhe. Spika: Mheshimiwa ulikwisha kuzungumza ndio nataka kuanza kujibu hayo mambo yenu. Waheshimiwa Wajumbe bahati nzuri serikali ipo yote hayo mmeyazungumza na yote hayo yana umuhimu. Mimi nitakachokifanya nitawapa mawaziri wanaohudika na hizo sekta ili waweze kutoa maelezo kidogo na nitaanza na Mhe. Waziri wa Afya kuhusiana na hilo lako Mhe. Jaku Hashim Ayoub ambalo ulilitoa juzi ili atupe maelezo kidogo.

Baada ya hapo nitampa Mhe. Waziri wa Fedha na suala la *ATM* ambazo hazifanyi kazi, lakini baada ya hapo pia nimpe Mhe. Waziri wa Miundombinu kuhusiana na suala la barabara na nitamalizia kwa kumpa Mhe. Waziri wa Kilimo kuhusiana na suala la mchanga na hiyo *scavator* iliyoko ili atupe maelezo. Kwa hiyo, nitaanza na Mhe. Waziri wa Afya kidogo Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru ni kweli kabisa juzi tulipokea hoja ya dharura ingawa haikuwasilishwa katika kufuata misingi yote ya kifungu cha 42. Lakini tumeipokea na tumeifanyia kazi na naomba sasa nitoe maelezo kutoka Wizara ya Afya ambayo yanayohusiana na maswali naweza kusema aliyouliza Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote kuwepo hapa leo tukiwa na afya njema na pili nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa miongozo yake, hekma zake, busara zake na maelekezo.....

Mhe. Spika: Naomba tusikilizane Waheshimiwa msikilizeni Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Afya: Na maelekezo anayotupa hususan katika Sekta ya Afya kwani yeye ni mtaalamu bingwa aliebobea katika sekta hii ya afya anaifahamu, ameshaifanyia kazi zaidi ya miaka 30 sekta hii na anaielewa vizuri sana. Kwa hivyo, tunaendelea kumshukuru kwa miongozo yake.

Pili naomba nitamke kwa sababu hii ni hoja ya dharura imetolewa kupitia Baraza lako naomba nitamke hivyo hivyo kwa niaba ya serikali kwamba naomba ieleweke kwa wananchi wote wa Zanzibar kama hoja ilivyowasilishwa hapa na haya itabidi tuwasilishe hapa hapa naomba ieleweke kwa wananchi wa Zanzibar kwamba hakuna jambo ambalo serikali halichukuliwi kwa uzito wake.

Naiomba ieleweke pia kwamba hakuna jambo serikali hii chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein inadharau ama kulichukulia jambo lolote kuwa jepesi na hasa katika sekta ya afya. Mambo yote haya katika sekta ya afya yamekuwa wakichukuliwa kwa uzito wake unaostahiki na tumepewa uzito mkubwa sana nilieleza katika *budget speech* ya mwaka huu kwamba tumepewa uzito mkubwa sana katika bajeti, tumepewa uzito mkubwa sana katika vipaumbele, tumepewa uzito mkubwa sana mimi na Waziri wa Elimu katika sekta hizi mbili kuu ambazo Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kwa mwaka huu ndio dira yake kuu kuziendeleza. Kwa hivyo, naomba kwa hoja hizi ieleweke kwamba Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar iko kwa ajili ya wananchi wa Zanzibar na sio kudharau ama kulichukulia jambo lolote kuwa jepesi.

Mhe. Spika, wakati tumepokea maelekezo yako ya hoja hii ya dharura kupitia kwa Mwakilishi aliewasilisha tulitafuta maana hatujapokea maandishi, kwa hivyo tulitafuta *hansard* na bahati nzuri *hansard* ninayo hapa. *Hansard* hii nimeisoma mimi na nime-*share* na wataalamu 10 wengine wanaoelewa masuala ya humu na masuala ya hospitali na wote wamesema hoja haijaelekezwa moja kwa moja, lakini tumeweza kupata vitu 3 katika hoja hii.

Kwanza kabisa ni suala la *lift* ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, *lift* ile ilikuwa kweli *maintenance agreement* yake imekwisha kwa muda wa mwaka mmoja na wakati tunapokea fedha *priority* yetu ya mwanzo kabisa kwa hospitali yoyote ya kwanza kabisa ni kuokoa maisha, kwa hivyo, fedha nyingi zilielekezwa kwenye maradhi ambayo ni makubwa na yanahitaji kuokoa maisha. Nakubaliana na Mheshimiwa na hayo aliyoyasema kwamba *lift* ni sehemu muhimu ya kupeleka mgonjwa na kumrudisha kutoka *theatre* na kwengineko. Lakini wataalamu waliona kwamba fedha hizi lazima kwanza ziende kutoa tiba moja kwa moja.

Katika mafungu yaliyopangwa mwaka huu katika fungu la kupandisha hadhi ya Hospitali ya Mnazi Mmoja basi fungu hili la *lift* nalo limo ndani katika mchanganuo wake. Kwa hivyo, kampuni ya kufanya *repair* ile *lift* ambayo inaitwa *OTIC* chini ya wawakala wao *East African Elevators* wametuletea mkataba wa milioni 35 shilingi ambazo ninazo ushahidi wake hapa tutazilipa hizo fedha na *lift* hiyo mara moja itaanza kufanyiwa kazi.

Lakini kwa upande wa *lift* ya pili ambayo ile lift ya pili inaweza kuisaidia hii *lift* mpya maana hii ni mpya ile nyengine ni kongwe ile lazima ibadilishwe mfumo wake mzima, tulikuwa tukisubiri kwa sababu mikataba miwili imeshasainiwa ya *DABEA* na mkataba wa *Kuwait Fund*, tulikuwa tunasubiri mkataba wa tatu wa Saud kwa sababu wale wanakuja *Saud Fund* pamoja ili matengenezo yale yaingie katika *General repair* ya jengo zima la Mnazi Mmoja Hospital na hayo yanasimamiwa na ndugu zetu wa Wizara ya Fedha. Naomba niendelee Mhe. Spika.

Hapo hapo natoka kwenye *lift* naingia kwenye mchanganuo wake wa pili ambao tumejitahidi kutafuta hoja nini anajaribu kutafuta Mhe. Jaku Hashim Ayoub tumepata la pili ni paa la Mnazi Mmoja kuvuja. Katika hilo suala la paa la Mnazi Mmoja kuvuja ni kweli linavuja na paa lile linahitaji matengenezo paa zima kuondoshwa na kuwekwa paa jengine jipya. Muda mrefu tulikuwa tukisubiri hii mikataba hii ya *Kuweit Fund* pamoja na hawa *BADEA* na *Saud Fund* ambao wako pamoja.

Mikataba miwili tumeshapokea tayari bado mkataba mmoja, lakini kwa umuhimu wa eneo hilo tumejadiliana tumekaa na nilitoa maelezo hapa kidogo katika *budget speech* ingawa muda haukuwa wa kutosha, tumejadiliana kwamba kazi hii tuifanye sisi wenyewe na muongozo wa serikali pia tumepata kwamba tufanye kazi hii sisi wenyewe bila ya kusubiri wafadhili ambao sasa hivi tumekuwa tukisubiri zaidi ya miaka mitatu. Kwa hiyo, kazi hiyo tutaifanya sisi wenyewe kwa kutumia bajeti yetu wenyewe na tutaiweza. Serikali hii haitoanguka daima chini ya uongozi mahiri wa Dr. Ali Mohammed Shein.

Mhe. Spika, la tatu lilikuwa suala la *X- Ray*, naomba nitamke wazi kabisa sisi pale tuna jumla ya *X-ray* 4. X- Ray moja *digital* jana nimezipitia tena kwa ajili ya uhakiki, katika jengo jipya majengo yale mawili yaliyojengwa ambayo yalifunguliwa mwezi wa Novemba mwaka jana na Mhe. Rais Dr. Ali Mohammed Shein na tatu ni ndogo ndogo ambazo zinaitwa mobile *X-Ray Unit* ambazo ziko chumba cha *X-Ray*.

Kile alichokiona Mhe. Jaku Hashim Ayoub kilichobandikwa ni pale walipoishiwa ni ile *toner* ya kusafishia zile *film* kwa sababu zile ni *consumable* ambazo zinanunuliwa kila mwezi na wakati mwengine katika *supply* huwa zinachelewa kufika. Kwa hivyo, huwa tunaishiwa na zile dawa za kuchangia ili kutoa filamu.

Kwa hiyo, kile kilichoonekana ni kukosekana kwa ile dawa lakini *X- Ray* zinafanya kazi na baada ya hapa mimi nitaomba mimi na Mhe. Jaku Hashim Ayoub tukapige *X-Ray* ya vifua sote wawili kwa pamoja kwa ajili ya kupata ithibati yeye apigwe kifua chake na mimi nipigwe kifua changu tutaziwasilisha picha hizo mbele yako.

Mhe. Spika. Ahsante sana naomba kuwasilisha majibu hayo. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Afya kwa maelezo yako. Mhe. Jaku Hashim Ayoub hakuna mjadala *please*, Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwanza naomba nichukuwe fursa hii kumshukuru sana Mhe. Mohammed Said Mohammed kwa kulieleza suala hili hapa Barazani. Lakini

nimjulishe tu na pia niwajuulishe Waheshimiwa Wajumbe kwamba *ATM* hizo kwanza sio mbovu na ni baadhi tu ambazo zilikuwa zina matatizo kwa jana na ni sababu zilizotokana na kwamba kuwa na usumbufu huo zilizidiwa. Matumizi jana yalikuwa makubwa watu wengi walikuwa wanahitaji fedha na walitumia huduma hizo za *ATM* kwa hivyo, zilizidiwa.

Sasa nilichukuwe suala hili tujue nini tunaweza tukafanya ili kuondoa usumbufu huo kwa siku zilizobakia kabla kufika siku ya sikukuu. Sina zaidi ya kusema zaidi ya hayo kwamba tunalichukuwa tutafanya utaratibu lakini pamoja na kwamba watu wengine wanapata huduma kwenye *ATM* bado wanaweza wakaenda Benki pale wakapata huduma kama hizo kupitia kwenye madirisha ya benki.

Lakini hili tunalichukuwa na jitihda kubwa zaidi inafanywa na benki kama nilivyowahi kusema hapa ya kuongeza idadi ya *AMT* hizi katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Nakushukuru Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Afya, sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji au Naibu wake suala la barabara la Mhe. Machano Othman Said.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, hapa nafikiri kulikuwa na suala linaulizia kuhusu bahari za njia zetu. Mhe. Spika, nataka nikuhakikishie na kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba baada ya mvua hizi zilizopita za masika njia zetu nyingi hapa Unguja na Pemba zimepata matatizo, bahati nzuri tukazitemebelea hizi njia na viongozi mbali mbali wamekwenda kutembelea njia na madaraja Pemba na hapa Unguja, ninachotaka kusema kwamba wizara ikishirikiana na wizara nyengine tuko katika kutengeneza mpango kabambe wa kushughulikia hizo njia.

Nimepata taarifa kwamba baadhi ya njia hizo mojawapo ni njia ya *airport* nadhani ishafanyiwa kazi

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mheshimiwa hatusikii.

Mhe. Spika: Mheshimiwa husikiki kidogo.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kwa ufupi ningependa kusema tu kwamba tumepata taarifa za matatizo ya njia na uhakika kwamba kazi inafanyika sasa hivi kurekebisha haya matatizo yaliokuwepo. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana naomba nimwite Mhe. Waziri wa Kilimo suala la mchanga *actual* ni *loader* sijui *scavator* ilioko kule Donge.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili na Mifugo: Mhe. Spika, awali ya yote naomba nikushukuru wewe na nimshukuru Mhe. Hassan Khamis Hafidh kwa taarifa hii ambayo ameileta kwenye Baraza lako tukufu.

Kwanza niseme tu kwa upande wa serikali ilipokaa pamoja chini ya Mhe. Mwenyekiti, hakuna pahali ambapo tumeagiza kwamba wale wafanyakazi pale waondolewe au wasipewe huduma hakuna agizo hilo hata siku moja.

Lakini la pili nimshukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma juzi alikuja akanipa taarifa hiyo anayosema Mhe. Hassan Khamis ikiwa pamoja na gharama kubwa ya hicho kijiko ambacho kinatoza. Hatua niliyoichukuwa ni kumuandikia....

Mhe. Spika: Waheshimiwa tusikilizane kidogo maana yake hatusikii. Pandisha sauti kidogo Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili na Mifugo: Ahsante, nirudie tena Mhe. Spika, kwanza nasema nataka kumshukuru sana Mhe. Hassan Khamis Hafidh kwa taarifa ambayo ameileta. Serikali kupitia kamati yetu inayoongozwa na Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Katiba na Sheria haijatoa agizo kwamba watu wale wanaofanya kazi pale waondolewe.

Juzi Mhe. Hamza Hassan Juma alikuja kunipa taarifa hiyo pamoja na kunieleza kwamba kuna gharama zinazotoza za ziada katika shughuli inayofanywa pale. Hatua niliyoichukuwa nilimuandikia Katibu Mkuu wangu dokezo nikimueleza yeye na Mkurugenzi waende waniletee taarifa leo Ijumaa ya mambo haya mawili.

Moja la kutumika kama hicho kijiko na gharama kubwa, lakini la pili hawa watu ambao wanafanyakazi wameondolewa kazini kinyume na maagizo ya kamati tuliyoagiza. Taarifa hiyo tunategemea tukimaliza shughuli hizi itakuwa imefika ofisini tutaifanyia kazi. Lakini nataka niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe, kila mnapopata taarifa kama hizi mtuambie, serikali iko makini na iko tayari kuyatatua matatizo haya kwa manufaa ya watu. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri. Katibu kwa shughuli inayofuata sasa.

UTARATIBU

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Spika, kuhusu utaratibu. Mimi nataka kujua kijiko kile ni cha nani ambacho kinaingiza shilingi milioni 17 kwa siku ni cha nani.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, nadhani Mhe. Waziri keshajibu kwamba ameshawatuma wataalamu wake watamletea majibu. Nafikiri ukitoka hapa utajua kila kitu. Mhe. Waziri yumo ndani humu na hao wataalamu wako nje, sidhani kama anaweza kuwa na jawabu hapa sasa hivi. Kwa hivyo, tusubiri akitoka nje utayapata majibu ya jambo lako. Katibu tuendelee.

HOJA ZA SERIKALI

Ripoti ya Utekelezaji ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar, Kuhusu Utekelezaji kwa Kipindi cha Oktoba 2013 - Disemba 2016

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwingi wa Rehma, kwa kutuwezesha kukutana katika Baraza lako hili tukufu, tukiwa katika hali ya uzima wa afya na kuweza kutekeleza majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Pia nawapongeza wajumbe wote wa Zanzibar kwa uweledi wao katika kufuatilia ripoti ya Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi. Kwa kuthibitisha hilo jitihada zenu zinaonekana wakati wa utekelezaji wa majukumu yenu katika kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwasilisha Ripoti ya Utekekezaji wa Kazi za Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, kwa kipindi cha Oktoba 2013 - Disemba 2016, kama ilivyoainishwa na kifungu cha 33 cha Sheria ya Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, nambari 1 ya mwaka 2012.

Mhe. Spika, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, ipo kwa mujibu wa Sheria namba 1 ya mwaka 2012, ambayo kifungu cha 13(1) kimeainisha majukumu matatu yafuatayo:

1. Kufanya uchunguzi dhidi ya vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi;
2. Kushauri Taasisi za Umma na binafsi juu ya namna ya kudhibiti mianya ya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi; na
3. Kutoa elimu ya umma kuhusu rushwa na uhujumu wa uchumi na athari zake kwa lengo la kushirikisha na jamii katika kuzuwia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi.

Muhtasari wa Ripoti

Mhe. Spika, ripoti hii inahusisha hatua zilizochukuliwa na Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, katika kukuza uelewa wa jamii juu ya athari za Rushwa na Uhujumu wa Uchumi.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tusikilizane kidogo. Tuendelee Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Katika kutekekeza jukumu hilo, mamlaka imetoa elimu kwa wananchi kupitia mikutano ya hadhara 227, vipindi 34 vya redio na televisheni vimerushwa hewani kwa kupitia *ZBC, TV* na redio. Vipeperushi vilitumika *poster* 10,000, machapisho na makala 50 zililenga katika kuongeza uelewa wa jamii kuhusu athari za rushwa zilichapishwa. Pia ofisi ilitumia maonesho mbali mbali ya ofisi inayotembelea kufikisha ujumbe kwa jamii unaohusiana na kazi na majukumu ya malaka.

Mhe. Spika, mamlaka inatumia pia mitandao ya kijamii, ikiwemo ukurasa wa *facebook*, *whatsApp* na barua pepe, njia ambazo watu wengi wanazitumia ili kurahisisha utoaji wa taarifa. Jitihada zinaendelea kwa kushirikiana na Tume ya Mawasiliano ya Tanzania pamoja na TAKUKURU ili kupata nambari za simu ambazo zinatumika na wananchi bila ya gharama yoyote kwa mtoaji wa taarifa.

Mhe. Spika, kuhusiana na tuhumu za vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, katika kipindi cha Oktoba 2013 hadi Disemba 2017, mamlaka imepokea malalamiko 268 yanayohusu vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi. Kati ya malalamiko hayo yaliyofanyiwa uchunguzi ni 184, na malalamiko 53 yalifungwa baada ya mamlaka kujiridhisha kwamba malalamiko hayo hayakuwa na hoja za msingi.

Jumla ya majalada 20 tuhuma zake zilipelekwa katika sehemu husika, ikiwemo Jeshi la Polisi. Aidha majalada 25 yalifikishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka na majalada 5 yamefikishwa mahakamani.

Mhe. Spika, mamlaka ilifanikiwa kufanya udhibiti wa vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi katika taasisi mbali mbali, likiwemo Shirika la Nyumba ambapo ilifanikiwa kuokoa jumla ya shilingi milioni 18,993,354. Udhibiti ulifanyika katika Bandari Kuu ya Unguja Malindi iliokoa jumla ya shilingi milioni 30,043,300. Aidha, mamlaka imeokoa kiasi cha shilingi 161,449,278.26 katika matukio mbali mbali na kufanya jumla ya fedha zote zilizookolewa kufikia 210,485,932.26.

Aidha, mamlaka imeendelea kushirikiana na *ZRB* kwa lengo la kudhibiti kodi, hatua ambayo ilisaidia sana katika kuwafanya baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu kulipa madeni yao kwa kupitia *ZRB*.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Oktoba 2013 hadi Disemba 2016, mamlaka iliwapatia mafunzo watumishi 98 kwa lengo la kuwajengea uwezo watumishi hao, ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Mafunzo hayo yalihusu mambo mbali mbali, ikiwemo mbinu za kisasa za kufanya uchunguzi, umuhimu wa udhibiti wa vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi, yaani fedha haramu na kadhalika.

Mhe. Spika, mamlaka ilifanikiwa kufungua ofisi mpya katika Wilaya ya Wete Pemba, pamoja na kuwapatia stahiki mbali mbali watumishi wake kama sheria na taratibu za utumishi zinavyoelekeza. Mamlaka kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo, imefanikiwa kufanya ununuzi wa vitendea kazi, thamani za ofisi, vyombo vya usafiri pamoja na matengenezo madogo madogo ya jengo la ofisi.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako pamoja na wajumbe wa Baraza, kwa kuipitia Ripoti ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi. Ni matumaini yangu kwamba michango yao, maoni yao na maelekezo yao yatasaidia sana katika kufanikisha mamlaka hii. Waheshimiwa Wajumbe, itasaidia sana katika kuimarisha utendaji wa Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa na Uhujumu Uchumi, pamoja na kuimarisha misingi ya utawala bora Zanzibar. Wizara ipo tayari kupokea ushauri,

maelekezo na miongozo hiyo na inaahidi kwamba itaifanyia kazi kwa nia ya kuifanya mamlaka hiyo kutimiza wajibu wake na majukumu yake ipasavyo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ili aje awasilishe na yeye ripoti yake.

Mhe. Machano Othman Said (Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): Mhe. Spika, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Bwana wa viumbe vyote, kwa kutujaalia uhai, afya njema na taufiki ya kuweza kukutana hapa leo hii, kwa ajili ya kutekeleza jukumu muhimu la kikatiba la kuisimamia serikali na kuwakilisha wananchi wa Zanzibar katika kufanya maamuzi muhimu ya kitaifa.

Aidha, nitumie fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili kutoa maoni ya Kamati yetu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusu uwasilishwaji wa Ripoti ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar kwa mwaka wa 2013/2016, kama Kanuni ya 43(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka 2016 inavyoeleza.

Mhe. Spika, nichukue pia fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuweza kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu. Ripoti ya Mamlaka ya Kuazuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi kwa kipindi cha mwaka 2013/2016. Ripoti hii inaakisi matokeo ya kazi za msingi zilizofanywa na Mamlaka hii tokea kuanzishwa kwake na kuanza kufanya kazi mwaka 2013, ingawa katika jamii zetu watu wengi hawajui maana halisi ya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, na jinsi athari zake zinavyodumaza maendeleo ya nchi yetu licha ya jitihada nyingi kuchukuliwa za kuwapatia elimu.

Mhe. Spika, kwa namna ya pekee napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe na makatibu wa Kamati hii ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kwa mashirikiano yao makubwa yanayoendelea na kuonesha ufanisi mkubwa katika kutimiza wajibu wake katika chombo hiki kitukufu katika nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba sasa kwa ruhusa yako niwataje Wajumbe wa Kamati yangu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kama ifuatavyo:-

1. Mhe: Machano Othman Said - Mwenyekiti
2. Mhe: Mwanatatu Mbarak Khamis - M/Mwenyekiti
3. Mhe: Wanu Hafidh Ameir - Mjumbe
4. Mhe: Saada Ramadhan Mwendwa - Mjumbe
5. Mhe: Suleiman Makame Ali - Mjumbe
6. Mhe: Nadir Abdulatif Yussuf - Mjumbe
7. Mhe: Ali Khamis Bakar - Mjumbe
8. Ndg: Rahma Kombo Mgeni - Katibu

9. Ndg: Ali Alawy Ali - Katibu

Mhe. Spika, aidha, nichukue fursa hii kuwapongeza kwa dhati kabisa viongozi na watendaji wote wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, kwa kazi zao nzuri na ngumu wazozifanya katika kusimamia haki na uchumi wa Zanzibar, licha ya changamoto mbali mbali zinazojitokeza na kukabiliana nazo.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo sasa naomba kutoa maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusiana na Ripoti ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar mbele yako kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, katika ripoti ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar ambayo hivi sasa ipo mbele yetu, Kamati inapata wasiwasi katika utendaji wao kwani Ripoti hii haioneshi mafanikio yaliyopatikana katika kazi zao kwa kipindi chote kilichopita kuanzia 2013 mpaka 2016. Aidha, Kamati ilitarajia kuona *ZAECA* imesaidia kuokoa kiasi gani cha mali za serikali, na vile vile wamesaidia kuokoa kiasi gani cha fedha za serikali kwa kipindi chote hicho ambacho kila siku matukio ya Rushwa na Uhujumu Uchumi yanaendelea.

Mhe. Spika, vile vile, ripoti hii inaonesha kuwepo kwa dosari katika muundo wa kiutumishi, kwani mpaka wakati huu Mamlaka ya *ZAECA* haijapatiwa muundo rasmi katika Idara zake, kutokana na muundo uliopo kuwa haujapitishwa rasmi na Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Hivyo kufanya Mamlaka kushindwa kutekeleza baadhi ya majukumu yake ya msingi kwa mujibu wa kifungu cha 13 cha sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa uchumi, Sheria namba 1/2012. Aidha, kamati inaagiza suala hili la muundo wa idara kushughulikiwa kwa haraka ili kuziba mianya ya watu wanaohujumu uchumi na kuingiza hasara serikali na jamii kiujumla.

Mhe. Spika, kupitia ripoti hii Mamlaka imeeleza kupokea taarifa na malalamiko kutoka katika vyanzo tofauti; Kamati yangu inashauri kupitia sheria ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, sheria namba 1/2012 kufanyiwa marekebisho ili kutoa ulinzi kwa raia wema wenye kutoa taarifa za wahujumu uchumi.

Mhe. Spika, lakini pia, Mamlaka iwe na uwezo wa kuwatia hatiani wenye kuvunja au kuficha taarifa za ukweli kuhusu waajiri ama wajiriwa wao. Kwa msingi huo itaweza kuwajengea imani watumishi ambao wako tayari kuwafichua watu wenye nia mbaya na maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, kamati yetu, katika ziara zake za kawaida iliwahi kufika katika Ofisi za *ZAECA* Unguja na Pemba na kutoridhishwa na mandhari halisi ya ofisi zao hususan Unguja. Hivyo, Kamati inashauri kuboreshwa kwa eneo lile la kazi ili kutoa fursa kwa watuhumiwa wakati wa kuhojiwa kuona wapo huru na salama kutoa taarifa. Vile vile, mahitaji yao yazingatie haki za binaadamu kwa kuzingatia utu wa mtuhumiwa husika.

Mhe. Spika, katika jadweli nambari saba (7) lilionesha tuhuma zilizoongoza kulalamikiwa mwaka 2013 – 2016. Kamati inashangazwa kwa kuona kuna asilimia

ndogo sana ya malalamiko ya Madawa ya Kulevya na mali zilizopatikana kwa misingi ya Rushwa, hali ambayo suala la Madawa ya Kulevya tumeona kila siku jamii inazidi kuathirika kutokana na uingizwaji na usambazaji wake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kamati inaipongeza Mamlaka ya *ZAECA* kwa kuwafichua na kupambana na wala rushwa katika nchi, ila cha kusikitisha ni kwamba, kazi kubwa na nzito hufanywa zaidi wakati wa kipindi cha uchaguzi kwa kuwatafuta wagombea wa CCM tu na kikimalizika nguvu yao nao humalizika. Naomba kurejea, kazi kubwa na nzito hufanywa zaidi wakati wa kipindi cha uchaguzi kwa kuwatafuta wagombea wa CCM tu na kikimalizika nguvu yao nao humalizika. Hivyo, kamati inashauri juhudi za kupambana na rushwa ziwe ni endelevu na zisiwe na ukomo wala wahusika wasichoke kusimamia na kufuatilia, ili kuweza kwenda sambamba na juhudi za viongozi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pamoja na hayo, kamati kupitia ripoti hii inataka kujua nani mwenye dhamana ya kusimamia sheria hizi, ikiwa mamlaka yenyewe inalalamikia kucheleweshwa kupitishwa kwa mpango wa kitaifa wa kuzuia rushwa na usimamizi wa maadili, ambao ulipangwa kuanza mwaka 2015 na ulitegemewa uende sambamba na dira ya maendeleo ya mwaka 2020. Mamlaka haioni kuwa kutosimamia ipasavyo sheria na mikakati iliyopangwa dhidi ya Mapambano ya kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi na kutegemea taasisi nyengine zishughulikie mipango hiyo kutaathiri utendaji wa kazi zao?

Mhe. Spika, zaidi ya hayo, kamati inashauri uchunguzi wa kina ufanyike ili kuweza kubaini wahujumu wa uchumi katika taasisi zote za Utumishi wa Umma, na kuwatia hatiani bila kujali cheo au nyadhifa ya mtuhumiwa husika. Vile vile, mtuhumiwa anapokana umiliki wa mali yake isiyohamishika, Mamlaka isiwe ndio mwisho wa uchunguzi wao bali waendelee kufanya uchunguzi mpaka pale mmiliki halali wa mali hiyo atakapo thibitika na kuchukuliwa hatua.

Mhe. Spika, sambamba na hayo, kamati inashauri Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi kushirikiana kikamilifu na Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, katika kuwaibua wahujumu uchumi ambao wanarudisha nyuma juhudi za serikali katika kupambana na umasikini ambao ndio kikwazo kikubwa katika maendeleo ya nchi yetu. Aidha, kamati inashauri Mamlaka ya *ZAECA* itoe elimu ya utoaji na upokeaji wa risiti kwa wafanyabiashara na watumiaji katika maeneo yote ya Zanzibar, ili kuepusha ongezeko la uhujumu uchumi.

Aidha, kamati inasikitishwa kwamba katika shehia zilizopewa elimu dhidi ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, hakuna shehia hata moja ya Mkoa wa Mjni Magharibi, mkoa ambao una watu wengi lakini mkoa ambao pia ndipo zilipo taasisi nyingi za umma na taasisi za watu binafsi.

Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini wakati ule nilipokuwa nikiwasilisha ripoti hii.

Mhe. Spika, mwisho kabisa naomba kuchukua nafasi hii kuwatakia Wazanzibari wote heri ya Eid-El-Fitri, na pia kuwapongeza kwa kufanya ibada na matendo mema katika

mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Namuomba Mwenyezi Mungu azikubali funga zetu. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nina wachangiaji wawili. Kwanza naomba nimwite mchangiaji wa mwanzo Mhe. Rashid Makame Shamsi, atafuatiwa na Mhe. Ali Suleiman Shihata.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi nikiwa mtu wa mwanzo kabisa kuweza kuichangia ripoti hii ya kipindi cha mwaka 2013 - 2017 inayohusiana na mamlaka hii ya Kuzuwia Rushwa na Uhujumu Uchumi.

Awali vile vile nimshukuru sana Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais anayeshughulikia Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ripoti hii ambayo imewasilishwa hapa na yeye akaiwasilisha kwa ustadi na uweledi mkubwa.

Vile vile nichukuwe fursa hii ya kuipongeza kamati husika chini ya Mwenyekiti Mhe. Machano Othman Said, kwa kuweza kutoa maoni yao juu ya ripoti hii. Niseme tu kwamba maoni ya kamati kama yatazingatiwa vizuri, basi tunaweza tukalipunguza kwa kiasi kikubwa sana suala la rushwa katika nchi yetu.

Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri akaitazama kwa kina ripoti ile ya kamati. Lakini pamoja na ripoti ya kamati na mimi nichukue fursa hii kuweza kuchangia machache kuhusiana na ripoti hii, pamoja na haya jana tulipokuwa tunajadili suala la madawa ya kulevya niligusa kidogo ripoti hii. Ripoti hii inavyoonekana zaidi imeelezea muundo wa taasisi yenyewe kazi zinazofanywa na taasisi hiyo, lakini vile vile imeonyesha takwimu mbali mbali naipongeza sana ripoti kwa kuweza kuyataja hayo. Lakini ripoti hii ina upungufu juu ya utendaji kazi hasa wa mamlaka yenyewe hawajaenda kwa kina juu ya utendaji kazi hasa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nilikuwa na maswali kwanza kuna taasisi ngapi katika suala zima taasisi imeeleza miongoni mwa shughuli zake ni kuweza kutoa ushauri wa taasisi mbali mbali juu ya udhibiti wa suala hili la rushwa. Ningependa Mhe. Waziri atakapokuja aweze kutwambia ni taasisi ngapi tokea 2013 zimepewa ushauri juu ya maswali yanayohusina na rushwa, lakini ni tathmini gani imefanywa kuona kwamba ushauru huu umesaidia au la. Kwa sababu inavyoonekana vitendo vya rushwa vinaendelea siku hadi siku kwa sababu inawezekana tunatoa ushauri lakini tathmini huwa hatufanyi kama ushauri ule unaleta manufaa au laa.

Mhe. Mwenyekiti, ndani ya ripoti hii kama alivyotangulia kusema Mheshimiwa Waziri kuna tuhuma nyingi sana zaidi ya 260, tuhuma hizi ziko katika maeneo tofauti zikiwemo wahujumu uchumi, ikiwemo matumizi mabaya ya mali za Serikali lakini vile vile mna tuhuma moja tu ya madawa ya kulevya ambayo niliisemea jana. Hii inatia mashaka sana na leo naleta msisitizo, kila siku ukisikiliza mawio maana yake kuna mtu kakamatwa na madawa ya kulevya hata hii leo asubuhi na wafanyabiashara wa madawa ya kulevya ni watu matajiri hawa kesi zao mara nyingi zinakuwa hazimaliziki na hazimaliziki kwa sababu ya tatizo la rushwa. Kwa hivyo wenzetu hawa wa mamlaka inayohusika wana

wajibu wa kuweza kuzifuatilia hizi kesi za madawa ya kulevya kwa sababu zimetawaliwa sana na rushwa, mimi nina imani Mhe. Waziri amesema wanawasomesha watu wengi hususam katika suala la uchunguzi, mimi ningeomba waanzie kuzichunguza hizi kesi wanaposikia kwamba kuna mtu kakamatwa na madawa ya kulevya basi watumie zile taaluma zao za kiuchunguzi kuzifuatilia hizi kesi zitafikia wapi. Kwa sababu kesi hizi zinaanza kuuliwa tokea ngazi za chini na tatizo kubwa sana linakuwa ni la rushwa.

Mhe. Mwenyekiti, takwimu hizi kwa kifupi zilizotolewa zinatia wasi wasi na zinatia mashaka kwa sababu kesi za madawa ya kulevya ziko nyingi, lakini vile vile kesi za wahujumu uchumi ziko nyingi. Lakini Mhe. Spika, ni kesi ngapi labda Mhe. Waziri kasahau ili atakapokuja atwambie ni watuhumiwa wangapi wa kesi hizi 260 angalau wangapi wameweza kufikishwa Gerezani kutokana na makosa yao ambayo wameyafanya. Kwa sababu kwenye kitabu humu mimi sikuona tunachokiona majalada yamefungwa, tunachokiona kesi zimehamishiwa taasisi nyengine sijaona kwamba kuna mtu ambae ametiwa hatiani na akafungwa mwaka mmoja miwili au mitatu kutokana na kesi za rushwa. Sasa hii sijui inatupelekea wapi kwa sababu inawezekana kuna tatizo katika uendeshaji wa kesi hizi.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ongozeko za taarifa ya mambo ya rushwa ambazo zinatolewa na watu binafsi, ndani ya ripoti hii inaonekana kuna ongezeko la watu binafsi kuweza kutoa taarifa zinazohusiana na rushwa katika kitengo hichi. Nichukue fursa hii kwanza kuwapongeza wananchi wote ambao wamethubutu kuweza kutoa taarifa za kirushwa katika kitengo hichi na naomba waendelee au tuendelee kwa sababu sote tunahusika na suala hili, pale ambapo tunaziona hizi kesi zinazohusiana na rushwa na tukaziripotia katika mamlaka inayohusika.

Lakini Mhe. Spika, katika suala hili la kuongezeka kwa taarifa zinazotolewa na watu binafsi ningependa numuulize Mhe. Waziri, je watu hawa wanalindwa vipi wanalindwa vipi kiusalama wao. Kwa sababu suala la rushwa ni suala la uadui, anihakikishie Mhe. Waziri ni jinsi gani watu hawa tunawalinda juu ya usalama wao ili wasije wakapata madhara kwa sababu kazi wanayoifanya ni nzuri sana, lakini je kuna motisha wowote ambao wananchi wanaotoa taarifa za rushwa wanapatiwa. Ningependa Mhe. Waziri atakapokuja aweze kutwambia kama kuna motisha yoyote ambayo tunawapa watu hawa kwa sababu mcheza kwao hutunzwa na hii ni kazi kubwa sana ya kuweza kuliondoa suala la rushwa.

Lakini la tatu Mhe. Spika, kuna kesi ambazo tunazisikia hata katika vyombo vya habari ambazo tunaambiwa kwamba pengine mtuhumiwa amekamatwa *red handed* humu sijaziona katika taarifa, lakini kwenye vyombo vya habari tunasikia askari wa usalama barabarani amekamatwa *red handed* na hizi katika mwaka huu mimi nimeshazisikia kesi tatu za *red handed* za usalama barabarani. Humu sijaziona sasa sijui inakuwaje kesi za namna hii humu hazitajwi na kama kesi mtu amekamatwa *red handed* kesi yake kwa nini isiweze kumalizika. Kwa sababu ushahidi ndio upo mtu amekamatwa na pengine ulitegwa mtego na waliotega mtego ni kati ya aliyetoa taarifa na wahusika wa mamlaka na pengine na askari. Lakini mwisho wa siku hatuoni kesi ambayo imemalizika ambayo pengine mtu amekamatwa *red handed* sasa hapa pana walakini, ningependa Mhe. Waziri

atakapokuja atueleze ni kesi ngapi za watuhumiwa waliokamatwa *red handed* na kesi zao zimefikia wapi.

Mhe. Spika, nikitoka hapo mimi nitoe ushauri tumeona kwamba kuna tatizo la uendeshaji wa hizi kesi na inawezekana zinauliwa kutokana na tatizo la rushwa, ningetoa ushauri kwa Serikali yangu tukufu ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kwamba kama hili tatizo tunalihisi ni kubwa basi tuanzishe Mahakama maalum inayohusika na wahujumu wa uchumi na vitendo vya rushwa, kama Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano alivyofanya maamuzi magumu katika hilo hii itaweza kusaidia kesi za wahujumu uchumi na rushwa zikaenda haraka na zikaweza kufahamika…

Mhe. Spika: Una dakika mbili Mheshimiwa.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, kama Serikali itaangalia suala hili la kuwa na mahakama au kitengo maalum cha kushughulikia kesi za namna hii nina imani kwamba kesi hizi zinaweza kwenda uadilifu na zikamalizika na tukaweza kuona manufaa ya kuweza kuliondosha tatizo hili la rushwa na wahujumu uchumi.

Mhe. Spika, pamoja na hayo nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri, kwa sababu kitengo hichi au mamlaka hii vile vile imeweza kuleta na kutoa au kufanya mambo ya manufaa kuweza kuokoa shilingi milioni 210 kwa hivyo tunaipongeza ni kitendo kizuri sana, lakini vile vile kuendelea kuwapa mafunzo vijana wake 98 ili waweze kukabiliana na kesi hizi. Lakini vile vile kuweza kununua vitendea kazi mbali mbali, lakini la kusikitisha Mhe. Spika, jengo la Mamlaka ya Rushwa haliridhishi Mhe. Spika, ningependa sana Serikali iweze kuangalia uwezekano wa ndugu zetu hawa wa Mamlaka kuweza kuwapatia jengo linaloendana na hadhi ya shughuli zao.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo na mimi naiunga mkono ripoti hii kwa kuletwa katika baraza na nawaombea kila la kheri kitengo hichi, au mamlaka hii kufanya kazi ili suala hili la rushwa liweze kupungua na hatimae kuondoka kabisa ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Rashid Makame Shamsi naomba sasa nimuite Mhe. Ali Suleiman (Shihata) atafuatiwa na Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame ameomba dakika tano, na Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ajiandaae.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na kuichangia ripoti hii ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi hapa kwetu Zanzibar. Lakini nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Mamlaka hii, na watendaji wake wote kwa kuhakikisha kwamba wanafanya kazi vizuri na wanaendelea kutuonyesha kwamba kuna kasoro zinazojitokeza katika maeneo mbali mbali ili udhibiti upatikane na kuondoa kasoro hizi na adha ya nchi yetu juu ya athari ya rushwa.

Mhe. Spika, rushwa ni adui wa haki na tunaambiwa tu kwamba mtoa rushwa na anayepokea rushwa wote ni maadui, kwa hivyo mimi kwanza ningeomba zaidi taasisi hii au mamlaka haya tuliyokuwa nayo wawe waangalifu katika kutafuta haki hiyo, rushwa ni

kurudisha nyuma maendeleo na ukiwa mkweli maendeleo yatapatikana kwa hivyo athari ya rushwa ni kuhujumu uchumi na kurudisha nyuma maendeleo ya nchi na kumkosesha mtu haki yake ambayo ni halali aifuate lakini kwa kuwa hana uwezo anaikosa haki ile bila ya matarajio. Kwa hivyo nimuombe Mkurugenzi wetu wa Mamlaka hii na watendaji wake wote wawe waadilifu na waendelee na kazi hii adhimu muhimu juu ya kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanakuwa salama pindi wanapodai haki yao juu ya kuendeleza maisha yao.

Mhe. Spika, kuna rushwa nyingi za aina nyingi kuna rushwa kwenye ajira mara nyingi vijana wetu wanatapeliwa sana kwenye ajira na mara nyingi wananchi wetu wanakosa haki zao wanapokwenda kuomba ajira. Leo tunasikia maeneo mbali mbali kwa mfano Polisi, JWTZ, Vikosi vya SMZ na sehemu nyengine utaambiwa kuna nafasi zinatoka wale wajanja wachache wanaambiwa nipe laki moja au milioni moja nikakufanyie mpango, kumbe mpango ule unakwenda mfukoni ile haki anayohitaji ya ajira ile anaikosa. Kwa hivyo niombe zinapotokea nafasi za kazi mara nyingi vijana wetu ndio wanapata athari za kuibiwa au kunyang'anywa bila ya kujitambua. Mimi ombi langu tu wakati ukifika kama hapo wenzetu Mamlaka wawe na watu wao ambao watakuwa tayari kujitokeza mle kwenda kufanya kazi ya kupata ule ushahidi wa mara moja, niiombe Wizara iongeze wafanyakazi, wafanyakazi wakiwa wengi na nchi yetu maeneo ni mengi basi haki itapatikana lakini pili naamini Mhe. Spika ukweli utajulikana.

Mhe. Spika, halafu suala jengine tunaloshindana nalo katika nchi yetu mimi husema tu kwamba masikini hana haki mwenye mali ndio mwenye haki na hii ndio maana ya kuwekwa tasisi hii kuwa ni Serikali ambayo inakwenda na utawala bora, niiombe serikali kwa makusudi sehemu za madawa ya kulevya ni hatari na sehemu za madawa ya kulevya Mhe. Spika kila vita tukivisikia vinaendelea lakini aliyefungwa aliyeshikwa humsikii. Kwa hivyo niombe serikali na niombe mamlaka haya masuala yaangaliwe kwa pande nyingi. Kuna ushahidi unakosekana kuna ukweli haupatikani kutokana na mtiririko wa mwenye fedha ndio mwenye uwezo, kwa hivyo kwenye madawa ya kulevya paangaliwe na hawa wahusika wafuatiliwe ili kesi zao zijulikane zinakwenda vipi.

Lakini jengine Mhe. Spika, katika mambo ambayo yanatuathiri katika nchi hii na kelele hizi zinaendelea siku hadi siku Mheshimiwa Mungu atuepushe sana na hichi kitendo cha udhalilishaji watoto wetu kina mama na watoto, hili suala lipo na linaendelea huwezi kukaa kwenye redio kwenye mawio ukakaa siku mbili usisikie mtoto kabakwa mtoto kafanyiwa udhalilishaji, lakini kesi hiyo haijulikani inavyokwenda. Kwa hivyo hapa panatumika ile ile rushwa kwa sababu kubwa linalotumika hapa ni uwezo wa pesa na uwezo wa kuharibu matokeo ya ile kesi ili mwenye uwezo afanye kazi zake. Nawaambia kama maelekezo ninayotoa au ushauri unapotokea udhalilishaji wa mtoto yoyote au mwanamke hata wanaume wanadhalilishwa wakati mwengine kwa hivyo ni vyema taasisi hii ikawa bega kwa bega na kile kitendo kilichotokea ili ukweli ukapatikana. Kwa sababu kama utamuachia mtoto wa watu kadhalilishwa nenda rudi nenda polisi nenda wapi siku mbili unaambiwa sisi ushahidi hatuna si kweli Mheshimiwa, mimi naamini uwezo wa fedha ndio unaohatarisha usalama wa vijana wetu na watoto wetu.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri hili liangaliwe na liangaliwe kwa uwezo mkubwa zaidi ili kuweka sawa na kuhakikisha kwamba wananchi wetu hasa vijana wetu na watoto wetu wanakuwa salama katika nchi yetu. Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa nia njema kabisa kaona pana haja na umefika wakati sasa hivi kuweka kitengo hichi juu ya kuhakikisha kwamba rushwa ni adui wa mambo mengi, hata unapokwenda hospitali siku nyengine unaambiwa kama huna chochote hufanyiwi kitu, haya yanawakuta wanyonge wetu. Kwa hivyo niombe tu hili liangaliwe na lipewe uweo lifanye kazi zake vizuri.

Mhe. Spika, kuna matatizo mengi ya elimu yaani taaluma, taaluma ni msingi wa mwanzo kuhakikisha kwamba vijana wetu na wananchi wetu hasa vijijini wanapata matokeo ya kujua na kuelewa, kwa sababu taaluma imetoa katika Mkoa wa Mjini Magharibi ni maeneo makubwa inasemekana yana rushwa lakini si mjini tu hata vijijini yamo. Kwa sababu sasa hivi ukuaji wa maendeleo katika nchi yetu mjini hupajui ukenda Kiwengwa unaambiwa mjini sasa hivi, ukenda Nugwi Mji, ukenda Kizimkazi Mji, kila utapokwenda ukenda pahala popote panapo mkusanyiko wa watu ni mjini.

Maana yake harakati tulizokuwa nazo sasa hivi Mhe. Spika, kama utakwenda ukanda wetu wa utalii utakuta kwamba mtiririko ulioko kule kuna hamasa kubwa ya maendeleo kuliko hata mjini watu wamedorora, kule watu wana kazi nyingi lakini peke yake na rushwa inatizamwa kwa macho mawili juu ya kutaka haki ambayo haina msingi upate kwa maisha yako. Mhe. Spika, kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri sehemu zote vijijini wananchi wetu wapewe taaluma ya kujua athari ya rushwa kutoa na kupokea, hiyo itatusaidia sana kuwaweka wananchi wetu katika maeneo mazuri.

Mhe. Spika, jengine nimesema rushwa ina eneo jingi au maeneo mengi kuna manung'uniko na yapo kweli vijana wetu wanaokwenda kuomba kazi hasa watoto wa kike mara nyingi wanadhalilishwa kwamba wanatakiwa rushwa ya ngono hiyo ipo, Mheshimiwa rushwa ya ngono ipo, anaambiwa mimi nitakupatia kazi lakini nataka kitu fulani ambacho ni hatari. Kwa hivyo nitoe wito na niiombe sana serikali katika sekta binafsi haya ndio zaidi. Ndio nikasema Mhe. Spika nakiomba hichi kitengo au mamlaka itafute wafanyakazi wengi ambao wasambazwe katika maeneo mbali mbali yatatusaidia juu ya kujua ukweli huu. Mhe. Spika, hakuna kuficha sasa hivi, tatizo hilo tunalo katika nchi yetu na lipo linaendelea na kuhatarisha maendeleo ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, katika mambo mengine kwa jumla niseme tu kwamba mimi naipongeza Wizara, naipongeza Mamlaka yetu hii ya Kuzuia rushwa na uhujumu uchumi, lakini nimuombe sana Mhe. Waziri umefika wakati wa kuwa wawazi mtoa rushwa na mpokea rushwa ni adui wa haki. Lakini yule mwananchi mwenye imani akasema mimi nimekwenda sehemu fulani nimeambiwa nitoe rushwa. Yule anakuwa hayupo katika salama katika maisha yake. Naomba sana pawe na ulinzi, pawe na usalama wa kumlinda mtoa taarifa huyu juu ya kuokoa maisha yake na haki yake ipatikane.

Mhe. Spika, baada ya hayo mchache mimi nasema tu kwamba naiunga mkono hotuba hii na naomba mawazo niliyoyatoa Mheshimiwa ayafanyie kazi ili kunusuru jamii yetu iishi

salama na hawa matapeli wachache wanaorudisha nyuma maendeleo yetu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa kupata wasaa huu kuzungumza machache kuhusu hoja hii ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba Sheria Utumishi wa Umma juu ya ripoti ya mwaka kuhusu utekelezaji wa kazi za Mamlakaya kuzuia rushwa na uhujumu uchumi.

Naomba nimshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Waziri kwa ripoti fupi lakini yenye takwimu muhimu sana. Mimi nimechukua dakika chache sana nimezipitia takwimu, kwa kweli zinajieleza wenyewe na kwa undani kabisa. Kwanza naomba niseme au nimnukuu Mhe. Waziri sijui kama yeye alisema lakini kwenye ripoti kwenye ukurasa wa 4 anasema:

> "Ili kutekeleza majukumu kwa utaratibu mzuri, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi *ZAECA* inatumia muundo usio rasmi wenye Idara kuu tatu. Idara ya Kinga, Idara ya Uchunguzi, Idara ya Utawala na Uendeshaji"

Sasa nikajiuliza kwa nini huo muundo uwe wa muda usiwe rasmi. Lakini zaidi anaeleza kwamba Idara hizi zisiwe rasmi kwenye muundo wa *ZAECA* bado muundo wake haujapitishwa rasmi na Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Chombo hiki kimeanzishwa tokea mwaka 2012 kwa sheria. Mamlaka ikaanzishwa mwaka 2013 miaka mitano leo bado chombo hakina utumishi, hakina muundo rasmi, kitafanya vipi kazi. Ina maana hakina meno kabisa, hii inajidhihirisha wazi na ripoti inasema vizuri kabisa ina maana haina meno ndiyo maana hawafanyi kazi.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tusikilizane, tumsikilize mwenzetu.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Zaidi ukenda kwenye ukurasa 16 zile takwimu aliyetoa Mhe. Waziri anasema kesi zilizopokelewa kwa jumla ni 268 uchunguzi umefanywa 184, zilizofungwa ni 53, taasisi nyengine 20, *DPP* zilizofika kwake ziko 25 zilizofika Mahakamani 5 tu sijui asilimia ngapi sijawahi kupiga. Sasa hii inajionesha wazi kwamba hichi chombo tumekiweka tumekipitisha hapa Barazani lakini hakijapewa meno, huo ndio ukweli hizi takwimu zinaonyesha na zaidi.

Mhe. Spika, hizi takwimu zake mimi nasoma takwimu zake Mheshimiwa, anasema tuhuma zinazoongoza kulalamikiwa ukurasa wa 19 kwenye ripoti anasema matumizi mabaya ya mali za umma kesi 72, matumizi mabaya ya ofisi kesi 57, kukwepa kulipa kodi kesi 44, kushawishi kuomba na kupokea rushwa kesi 43, rushwa katika zabuni kesi 12, rushwa katika uchaguzi kesi 9, kumdanganya mwajiri kesi 4 Matumizi mabaya ya mali na mapato 4, rushwa ya ngono 3, mali zinazopatikana kwa misingi ya rushwa 2, madawa ya kulevya 1, utakasaji wa fedha haramu 1.

Kwa hivyo kazi zipo Mhe. Spika, taasisi kwa mujibu wa sheria yao wafanyakazi lakini kama Utumishi wa Umma hawaitambui hii Mamlaka bora tuifute, Waziri alete sheria hapa tubadilishe sheria imewekwa kama *redundant* maana tumeweka chombo kifanye kazi lakini chombo hakifanyi kazi kwa sababu hatujakihalalisha wenyewe.

Mhe. Spika, naomba nimalizie nitafiti mimi naomba nimalizie, nilitafiti mimi kwa nini kesi hizi tano hizo nyengine zote hazijafanya kazi ipasavyo, kuna mgogoro mdogo sana ndiyo pale niliposema inaelekea kama hichi chombo kinapigwa vita. Mahakama Kuu hawazitaki kesi za Wahujumu uchumi, huo ndio ukweli, utafiti nilioutafuta wanapinga kesi wasizihukumu wao. Huo ni ukweli tumefanya utafiti na ndiyo maana hakuna kesi hata moja iliyohukumiwa.

Mhe. Spika, mimi namuomba Mhe. Waziri bora akafanye kazi vizuri na hichi chombo atafute kwa undani hasa *what is really problem* kunachemka nini, kwani chombo kizuri kama hichi kina kazi nzuri hakifanyi kazi. Mheshimiwa mimi naunga mkono ripoti na namtakia la la heri Waziri. Ahsante.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini. Sasa naomba kwanza nimwite Mhe. Panya Ali Abdalla atafuatiwa na Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, halafu anamalizia Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na Mhe. Panya Ali Abdalla karibu.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kunipatia nafasi hii niweze kusema machache katika chombo hichi muhimu cha Mamlaka ya kuzuia rushwa.

Mhe. Spika, kwanza nianze kumpongeza Mhe. Waziri yeye pamoja na watendaji wake lakini pia nianze kukipongeza Kitengo hichi Mamlaka hii Mkurugenzi na watendaji wake wote kwa kazi kubwa lakini ngumu kabisa ambayo haifikii katika yale malengo ambayo tumeyakusudia.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze kuchangia katika haya majadueli ambayo yanaonekana kuanzia mwaka 2013, kesi zinaripotiwa lakini mwisho wake kwenye kupokewa hizo kesi na muendelezo lakini na huo muendelezo wake inakuwa kama zilipokelewa nyingi ikiende katika muendelezo zinaanza kupungua. Lakini ikiendelea tena zilizofungwa majalada yaliyofungwa hapo ndio panapokwama. Ukija ukitafuta zilizopelekwa kwa *DPP* au zilizofikishwa Mahakamani huko ndio mwisho wa shughuli, hamna kesi ambazo na kama utazikuta kwa mfumo ulioanza kama kuna 10 basi unaweza ukaikuta moja tu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli katika wimbi hili itakuwa bado kuna tatizo kubwa sana kwa sababu kama tunavyoelewa mwenzangu aligusia kesi za madawa ya kulevya, kesi hizi tunazisikia kwa kweli nyingi na zinatusikisha kuona vijana wetu wanaendelea kuathirika na madawa na kesi zinakamatwa na mpaka zinafikishwa Mahakamani halafu unasikia kielelezo kimepotea Mahakamani, hili ni jambo la kusikitisha sana.

Mhe. Spika, tuseme bado kesi hizi hazijafanyiwa kazi ipasavyo ili tukaweza kufikia lile lengo la kuundwa hasa hii taasisi ili ikaweza kutusaidia wananchi na ikaweza kuwapatia haki wale wenye haki.

Mhe. Spika, utaona kuna kesi ambazo zinaelezwa hapa migogoro ya ardhi. Mheshimiwa tunasikitika sote hapa migogoro ya ardhi inakuwa ni mengi. Lakini ukijakuangalia katika ufikishwaji wa Mahakamani hamna. Sasa mgogoro huwo kweli ataweza kukwamuka katika mgogoro huo wakati haifiki katika ile haki ya maamuzi yakaweza kupatikana maamuzi ikajulikana kweli hapa pahala ni pa nani na nani anathibitika kuweza kumiliki mahali hapa. Mhe. Spika, bado niseme kuna tatizo kubwa.

Mhe. Spika, kuna suala zima la uajiri, katika sehemu hii ya uajiri ndipo hasa niseme ziliko hizo rushwa. Katika sehemu ya uajiri watu wanatumia nafasi hii kuwapatia watu kazi kwa kupokea mapato fulani. Mimi nilikuwa naomba na nasisitiza hichi kitengo hebu kijikite sana katika sehemu hii ya uajiri ukizingatia zikija zile ajira za vikosi watu wanachukuliwa pesa zao kudanganywa utapata kazi kesho, utaajiriwa keshakutwa, watu wanachukua pesa na matokeo yake wala mtu huyo hapati kuajiriwa. Sehemu ya uajiri bado huko wajikite sana katika kuona suala zima la rushwa linapatikana huko.

Mhe. Spika, niseme kwa wale wenye kutoa taarifa watu wenye kutoa taarifa ni watu muhimu sana ili kuzipeleka taarifa hizo ziweze kufanyiwa kazi. Watu hawa wanapoona tarifa walizozitoa hakuna hukumu zilizotolewa au hakuna hatua yoyote iliyofikiwa watu hawa wanavunjika moyo na si rahisi tena kuweza kumpata kutoa taarifa nyengine. Anahisi anapoteza wakati wake bure kulifuatilia suala hili mpaka linafikia ukingoni lakini mwisho wake hapati ule umalizikiaji wake limemalizikia vipi, jambo linamalizikia katikati huwezi kujua kama kesi hii ilikwenda lakini matokeo yake yamefikia hapa. Hapo ndio utaweza kujiridhisha au kesi hii imekosekana ushahidi wa kutosha imemalizikia hapa. Lakini inamalizikia katika kupelekwa na muendelezo na hajui hata hicho kinachoendelea ni nini.

Mhe. Spika, kuna suala zima la ubadhirifu wa mali za Umma. Suala hili linatuumiza na kama kweli hafikiwi mwisho wa kujua wenye kufanya ubadhilifu wa mali za umma hukumu zake hazipo. Nchi yetu bado itaendelea kuwa katika hali duni ya mipango ya maendeleo kwa sababu kinachopatikana watu wanakihujumu. Hili ni suala ambalo litakuwa linakwamisha misingi mikuu ya serikali ambayo inayowapatia huduma wananchi wake.

Mhe. Spika, pia kwa hawa watu wanaotoa taarifa mimi ningeomba watu hawa wanaotoa tarifa kuwapa motisha ni kitu muhimu pia kwa sababu kuna taarifa nyengine zinakuwa nyeti kabisa huwezi kuipata taarifa hiyo kwa sababu mtu kama anajitolea muhanga kwa sababu kuitoa na wewe unaweza kama hasa hizi taarifa za madawa ya kulevya. Madawa ya kulevya unaoshindana nao ni watu wenye fedha nyingi sana kwa hivyo wanapotoa ile taarifa pia na wao kuweza kuwapa hifadhi fulani.

Mhe. Spika, mimi nitaka nichangie hayo kwa kuona umuhimu wa hii taasisi, lakini Mhe. Dkt. Mwinyihaji pale ameeleza kama hii taasisi bado hatujaitendea haki hatujaipa meno hasa ili ikaweza kufanya kazi zake ipasavyo. Mhe. Spika, naomba hilo lifanyike lakini hata jengo zuri la kuweza kuonekana hawa watu ambao wanataka kutoa hukumu kwa watu wenye fedha mbali mbali lile jengo lao haliendani na hadhi hiyo.

Mhe. Spika, ni kitu cha kuzingatia lazima lipatikane jengo zuri ambalo kweli hii taasisi ionekane inashughulikia masuala haya makubwa kwa sababu suala la rushwa ni suala kubwa kwa sababu ni fedha inayotumika.

Baada ya kusema hayo mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja ripoti hii lakini pia iombe na nisisitize yale yanayopatikana hasa ubadhirifu wa mali za umma, ukwepaji wa kodi, Migogoro hii ya ardhi ambayo haichukuliwi hatua hivyo ni vitu ambavyo navisisitiza sana viweze kufanyiwa kazi ili kila moja aweze kupata haki yake kama inavyopaswa. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Spika: Sasa nimwite Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali atamalizia Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa dakika tano.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii kuchangia machache juu ya ripoti ya taasisi yetu hii. Niseme kwamba tunapoangalia yale melengo na kazi zao kwa kweli lazima tuipongeze taasisi hii kwa kuweza kufanya kazi zake vizuri, katika maeneo yake yote matatu. Maeneo ya kutoa elimu kwa Jamii ili jamii ishindikane na iachane na tabia hizi za kupokea rushwa na kuhujumu uchumi.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo muhimu sana kulielewa kwamba tendo hili la kutoa rushwa ni tendo la siri kubwa sana. Kwa maana hiyo wafanyakazi wa taasisi hii hawapo kila pahali kwa hivyo sisi wananchi, sisi viongozi tuna wajibu wakati wowote kuisaida taasisi hii kwa kutoa taarifa za siri na zenye ukweli ili zifanyiwe kazi. Tukigeuka sisi kama ni watizamaji na tukaifanya taasisi hii kama wachezaji kwa kweli tutaendelea kuilaumu siku hadi siku. Nadhani wakati wamefika sisi viongozi kuwa mstari wa mbele kutoa taarifa, kuwa mstari wa mbele kuelimisha jamii juu ya suala la rushwa na madhara zake pamoja na uhujumu uchumi.

Mhe. Spika, niseme kwamba katika kipengele cha kazi moja ya msingi ya taasisi hii ya elimu kwa kweli hapa taasisi hii imefanya kazi vizuri na niseme tu iendelee kufanya kazi vizuri. Msingi hasa wa taasisi hii uko zaidi katika kuzuia katika kukinga na hapa kwenye elimu ndio kwenye kukinga yaani tunaielimisha jamii ubaya na kuachana na suala hili.

Lakini hata hivyo tuelewe kwamba suala la elimu ufahamu unakwenda pole pole hatutarajii mafunzo waliyotoa mwaka jana ya kuweza kuleta athari leo. Lakini tunaamini baada ya miaka minne mitano watu watakuwa wanaelimika. Hii inafafana kama na mawaidha ambayo tunayapata katika dini zetu, sio kwamba unaambiwa leo unafahamu leo unakuja kufahamu baada ya miaka minne mitano ala! kumbe nimeambiwa jambo fulani kumbe ni baya. Na huu ndio utaratibu wa elimu hizi za mwamko zinakwenda hatua kwa hatua.

Mhe. Spika, tujiulize hivyo wangapi kati ya sisi Wawakilishi tunaiondoa hii rushwa kwa mikono yetu. Lakini pia tujiulize wangapi sisi Wawakilishi ambao tunaikemea hii rushwa na wangapi tunaichukia. Kwa kweli jawabu tutakazopata ni tofauti, nadhani sasa wakati

umefika kuiondoa rushwa kwa mikono yetu, kuikataa katika mazingira yetu kuikataa katika taasisi zetu, kuikataa katika vijiji vyetu na mitaa yetu rushwa za aina zote. Haifai hata kidogo kushabikia ngono ya aina yoyote iwe ya rushwa, awe ya ajira, iwe ya muhali au nyengine yoyote. Lazima tusimame mstari wa mbele kuipiga vita. Hii nasema kwa sababu watoa rushwa wanatoka katika jamii tunayoishi nazo, kwa hivyo ni dhahiri wanajulikana kwa majina yao wanajulikana kwa mitaa yao, wanajulikana kwa vijiji vyao, lakini pia wanajulikana hata wapenzi wao. Lazima kuanzia sasa tucheze kwa maana kwamba tuiondoe rushwa hii, tusiwaache peke yao ZAIKA na sisi tunahusika. Nadhani kwamba kwa zumari hii iliyopigwa nadhani pepo atapanda kichwani tuiondoe rushwa. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Sasa naomba nimalizie na Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto dakika tano.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba nichukue nafasi hii na mimi pia kukupongeza na kuchangia ripoti ya mwaka ya kuhusu utekelezaji wa kazi kwa kipindi cha Oktoba 13/16 ya masuala ya rushwa.

Mhe. Spika, mimi ingependa nizungumze kwa ujumla zaidi kwa sababu naona kuna mambo mengi ambao yanagusa sana Wizara yetu na hayo ndiyo yanayosababisha kwamba sisi Wizara yetu isiweze kufikia hatua ya kuweza kuhukumu kesi na kuzitafutia mahali zinapotakiwa kwa sababu tu kuna hizo chembe chembe zinazoitwa rushwa. Rushwa hizi namna ya kuzipata ushahidi wake inakuwa ngumu.

Kama tunavyoona kwenye *page* ya 16 inasema kesi zilizofunguliwa utaona ni nyingi Mheshimiwa lakini zilizopelekwa Mahakamani ni 5 tu. Lakini pia ingependekeza kama inawezekana kuwe na *column* ya kuonyesha kwamba zilizohukumiwa, waliohukuwa ni watu wangapi. Utaona katika sehemu nyingi utaona nyingi zimeishia kwenye Mahakama, lakini ukiangalia pia namna ya kuwapata hawa watoa rushwa kwa sababu mtoa rushwa anakuwa ni msiri na anayepokea rushwa naye pia anakuwa ni msiri. Masuala haya yanakuwa ni magumu kwanza.

Mimi nimejaribu hata kuona kwamba kuna kitu kimoja mimi nakiita siku zote bima ya rushwa. Bima ya rushwa inatuumiza sana hata sasa hivi tukiwa kama ni viongozi inawezekana ukaanza kuweka bima ya rushwa kwa ajili ya uchaguzi ujao, kwa ajili ya kuomba kazi, kwa ajili ya kutaka kupeleka watoto shule kwa sababu utaanza kumjengea mazowea mtu yule ambaye unahisi kabisi siku moja atakufaa.

Tayari umekuwa umeshaweka bima ya rushwa kwa hivyo ukishaenda kwake wakati una hali halisi huna haja ya kutoa *cash* ni ile tuu kwamba umeshafika na kila siku unamfadhili unakwenda unafika vituoni polisi unazowea viongozi pale, unazowea watendaji, unakwenda hospitali unazowea yale mazoea tayari unakuwa umeshaweka bima ya rushwa ambayo siku moja itafanya kazi.

Sasa hivi ukiangalia tunapiga kelele na viongozi wote wakuu wanapiga kelele suala zima la rushwa, lakini hebu hawa watu wa TAKUKURU wajaribu kupeleleza bima za rushwa jinsi gani zinaanza kuandaliwa, zinaandaliwa katika maeneo yote na ukiangalia kwetu kunaa suala zima la rushwa ya muhali, inafika kesi zinakuja kwenye wizara yetu tunakwenda mahala fulani lakini kuna rushwa ya muhali mtoto wa mjomba, mtoto wa shangazi, huyu ni ndugu yangu na nini hapa panapita mazingira ambayo yanakuwa hayawezekani kabisa kumchukulia mtu hatua.

Au vyenginevyo wale wanaoleta kesi za kutaka kuleta sehemu zetu kwa mfano ofisini familia inakaa wanamtisha na yule ambaye anahusika na ile familia usipoacha hii tunakusomea halbadiri, usipoacha hivi sijui tunakutenga kwenye familia na utaona lile ni kosa la mtu yule pale anafika pahala hawezi na ameshatishwa hana jinsi ya kufanya anabaki anahangaika. Mimi naona bado hizo ni rushwa, kwa mfano kulikuwa na kesi ambayo alitolewa mtoto ameumizwa baba yake akatishwa kabisa akaja mtoto na familia nzima ofisini kusema kwamba sisi tunataka yaishe haya na wakamwambia usipokubaliana na sisi tunakuroga utakufa.

Lakini mtoto ananinong'oneza mheshimiwa nimeambiwa mimi baba afute kesi hii kwa sababu nitapewa shamba, mtoto wa miaka saba anapewa shamba atalijenga lini au nyumba kiwanja cha kujenga nyumba maisha yake miaka 7 hajaenda shule, anapewa rushwa ya namna hiyo anategemea atafikia wapi. Lakini ukiangalia kwenye ukurusa 19 tena na 18 yote nayo inaonyesha kabisa kwamba kunakuwa na taarifa zinaripotiwa nyingi lakini inapofikia mwisho ni ndogo kabisa inaonesha kama kwamba hata namna ya kufikia lile lengo la kuweza kudhibiti haiwezekani.

Lakini pia kuna rushwa ya ngono watoto wetu wa kike wanateseka sana wanapo kwenda kwenye maofisi, wanakwenda kabla hawajafanya *interview* wataitwa sehemu za pembeni wakaambiwa maneno yasiyokuwa na maana na mara nyengine wasiponiona fanya hivi sikupi sijui wanafanya nini wanateswa katika sijui watu wa rushwa watatusaidia katika masuala haya.

Wengine wanasema matumizi mabaya ya ofisi, matumizi mabaya ya ofisi unajua kabisa mimi niko hapa ofisini na mimi ndio mwamuzi wa mwisho unasema usipopatana na mimi hupati kitu tayari ni rushwa ile, unamtisha kwanza ni *sexually harassment* ni hali halisi ya kumfanya mtu akakosa amani na akashindwa kupata haki yake.

Lakini kuna suala la kushawishi na kupokea rushwa hizi zinatokea sana kwenye maeneo ya watu ambao tunapopeleka ripoti taarifa, mtu anakuzungusha. Mtu anakwenda kupeleka kesi ya kutaka kusaidiwa ya udhalilishaji atakwambia njoo kesho ataambiwa sijui na nini, tuonane baadaye akiona hajapewa rushwa ile kesi inaishia mahali haileweki inaenda wapi.

Jengine ningependa tu kusema kwamba tuendelee kushirikiana sana na Jeshi la Polisi kwa sababu Jeshi la Polisi tunalitegemea sana, na ni watu wa mwanzo wanaopata wanaaopata taarifa zinatokea kwenye jamii, sasa ikiwa wao hawatatusaidia na wakawa

ndio mwanzo wa kuonesha dalili za wale wasiokuwa na maadili masuala ya kutaka kupata rushwa inatukatisha sana moyo.

Lakini pia kwenye masuala la afya waendelee kuelimisha watu kwamba ni muhimu kwenda kutembelea huko ili waweze kupata elimu ya afya. Na katika masuala ya elimu nimeona kwamba wahusika wamepeleka sana katika sehemu mbali mbali ya ofisi wizara mbali mbali zimetembelewa lakini ningependa kutoa wito tuu ya kusema kwamba Kitengo cha Rushwa kisemwe sana kwenye jamii iwe wazi katika vipindi vyote na vikiwezeka vitolewe wazi viweze kuwekwa tuwe wazi. Lakini kuna maswala mengine ucheleweshaji wake muda ni mwingi mno...

Mhe. Spika: Mheshimiwa dakika tano umeomba dakika tano.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mheshimiwa naomba tu niseme kwamba mimi napenda kuiunga mkono hii hoja iliyoletwa lakini utaratibu wake uwe ni mwepesi watu waweze kuchukua hatua.

Mhe. Spika: Ahsante sana naomba sasa nimwite Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili ahitimishe.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, nashukuru Mwenyezi Mungu kujaalia kupata nafasi hii tena kuja kutoa ufafanuzi wa mambo mawili matatu.

Lakini nikushukuru sana Mhe. Spika na niwashukuru waheshimiwa wote waliochangia ripoti yetu hii jumla ya waheshimiwa waliochangia ripoti yetu ni saba.

1. Mhe. Machano Othman Said
2. Mhe. Rashid Makame Shamsi
3. Mhe. Ali Suleiman Ali
4. Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame
5. Mhe. Panya Ali Abdalla
6. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
7. Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto

Mhe. Spika, lazima tukubali kidogo na turudi nyuma kidogo kwamba hii ni ripoti yetu ya mwanzo na Mhe. Spika utakuwa umeweka historia kwamba ni Spika wa mwanzo ambao katika kipindi chako imewasilishwa ripoti hii kwa mara ya mwanzo.

Kwa hivyo ni jambo ambalo ni jipya tunahitajia kupata ushauri kama tulioupata hapa na ninashukuru waheshimiwa wametoa ushauri mzuri sana. Chombo hiki tokea kiundwe hivi sasa kama alivyosema Dk. Mwinyihaji ni kweli inakaribia miaka mitano na bahati nzuri katika miaka mitano hii, miaka mitatu na nusu tulikuwa chini ya mamlaka yake vile vile na wakati ananikabidhi idara hii alinikabidhi nashukuru Mwenyezi Mungu pamoja na tatizo hili la muundo alikuwa anajua kwamba kuna tatizo.

Lakini nashukuru nampa taarifa rasmi kwamba tayari serikali ni juzi tu ishatoa muongozo na muundo kamili wa idara hii sasa hivi ishaundwa, kwa hivyo ziko tayari idara tatu katika kitengo chetu hiki cha rushwa.

Aidha, naomba nichukuwe nafasi hii mheshimiwa nikiri kwamba jengo pale mahali lilipo lina matatizo ni mahali ambapo panawapa tabu wananchi kwenda kutoa taarifa zao wakati mwengine kwasababu ukienda pale kwanza utakuwa na wasiwasi unaonekana kama unaonekana pako wazi mno lile jengo linahitajia kuwa mahali pazuri pastara mimi niliwahi kufanya ziara nikaenda nikakagua jengo lile, baada ya kulikagua nikawashauri tuanze kutafuta eneo jipya la kujenga jengo la kisasa litakalokidhi mahitaji. Kwa hivyo jambo hili tunalipokea na namshukuru sana Mwenyekiti kwa kutoa taarifa hiyo ya kwamba jengo linahitajiwa kufanyiwa marekebisho Unguja na Pemba na tutafanya hivyo tukijaaliwa.

Lakini pia kazungumzia suala zima la mapato katika ripoti yake nimeona, mapato tumeeleza kwamba jumla ya shilingi milioni mia mbili na kumi na zaidi hivi zimepatikana au zimeokolewa kwa hivyo kwenye taarifa suala hili limo limejieleza vizuri sana lakini labda mengine hayakujitoshekeza kama inavyohitajika lakini kwa kweli tunashukuru sana.

La tatu alilozungumza kwamba Idara yetu hii au kitengo chetu hiki kinafatilia sana rushwa wakati wa uchaguzi kwa wanachama wagombea wa CCM tuu. Sasa niseme bahati mbaya labda Mhe. Machano na wengineo wote pengine wewe ndio uloeleza *concern* hii kwamba inafata CCM mimi napenda nikuhakikishie kwamba hawafwati CCM.

Lakini suala hili linakwenda na kutoa taarifa kuna hivi kwa sababu jambo hili lazima liwe na mashirikiano ya pande zote mbili, sisi kama upande wetu wa kitengo chetu kikishapata taarifa ni kufatilia na wao wanafanyakazi na kwa kweli hii ni mara yetu ya mwanzo tumeanza kufanya kazi hizi. Lakini nataka nikuhakikisheni kwamba katika chaguzi hizi zinazoendelea hatuangalii wa CCM hatuangalii wa yoyote.

Yoyote ambaye atatoa ambaye rushwa kwa njia yoyote ile atabanwa kwa sababu vijana wetu wamesambazwa maeneo yote sasa hivi sikumbieni wapi na wapi lakini wamesambazwa. Kwa hivyo wale ambao wanajitayarisha kwa ajili ya 2020 wajue tuu kwamba hili jambo wawe makini sana katika hali yoyote ile hatutokubali na kiongozi yoyote anakayetoa rushwa chama kinashotoa maelekezo mwenyekiti keshatoa maelezo hatokuwa na nafasi ya kurejeshwa kwenye nafasi yake.

Kesi za ardhi Mhe. Panya anazungumza nadhani hapa tuelewane kwamba kesi za ardhi huwa zinapelekwa kwenye Mahkama ya Ardhi kwa hivyo jambo hili liko kwenye Mamlaka ya Mahkama ya Ardhi, lakini kama kuna suala la rushwa kama hatukuletewa taarifa kitengo kile hakiwezi kutoa jawabu yoyote lazima tuletewe taarifa na hapa ndipo panapokuwa na mtihani hatupati mashirikiano ya kutosha watu bado wanahofu hofu kidogo kutoa taarifa hizi.

Mhe. Shamsi alisema kwamba taasisi zilizotoa ushauri ni ngapi ni sita tayari zishapewa ushauri kwa jambo hilo jee, tathmini inafanywa iwapo ushauri uliotolewa au laa jibu ndio unatolewa ushauri ule unaofaa. Halafu watuhumiwa waliotiwa hatiani hakuna hukumu iliyotolewa hadi sasa ingawa kuna kesi tano mahakamani na majadala karibu 25 hakuna kesi iliyotolewa hukumu.

Dk. Mwinyi amezungumzia suala zima hapa kwamba kunja tatizo hapa Mahkama Kuu hawataki kutoa hukumu yao kwasababu hawataki kesi za rushwa hili nimemsikia sasa hivi mimi nitalifanayia kazi kwa nguvu zangu zote tuone kuna tatizo gani ili tutowe suluhisho tukijaaliwa.

Mhe. Mmanga Mjawiria, Mhe. Castico nawashukuru sana wamenisaidia sana kutoa ufafunuzi wa masuala mbali mbali napenda niwahakikishie kwamba ushauri wao na msaada wao nimeuthamini sana na *Inshaallah* tukijaaliwa tutaendelea kushirikiana.

Mhe. Spika, naomba nitowe kwa muhtasari haya ni maelezo lakini ushauri tumeupokea jambo hili ni jipya tunahitaji kulifanyia kazi tuwe makini sote tushirikiane viongozi wote tulaani na kupambana na wahujumu uchumi pamoja na wala rushwa. Ahsante.

Mhe. Spika: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwahoji wale wote ambao wanaopokea ripoti wanyanyuwe mikono, wanaoikataa ripoti, imepolekewa waheshimiwa. Katibu shughuli inayofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi namba 3 ya 1985 na Kuanzisha upya Mahakama ya Kadhi na Kuweka Masharti Mengine yanahusiana na hayo

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi namba 3 ya 1985 na kuanzia upya Mahakama ya Kadhi na Kuweka Masharti Mengine yanahusiana na hayo kusomwa kwa mara ya kwanza.

Mswada wa Sheria Kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria Kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo kusomwa kwa mara ya kwanza.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Katibu: Mhe. Spika napenda kulitaarifu Baraza lako Tukufu kuwa shughuli zote zilizopangwa katika Mkutano wa Sita wa Baraza la Wawakilishi zimemalizika.

Mhe. Spika: Ahsante naomba nichukuwe nafasi hii waheshimiwa wajumbe sasa nimwite Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ili aje afunge Baraza. Mheshimiwa karibu sana.

KUAKHIRISHA BARAZA

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, mwenye wingi wa rehma, muumba mbingu na ardhi na vilivyo ndani yake na kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kufika hapa leo hii baada ya kufanikisha vizuri Mkutano wa Sita wa Baraza hili Tukufu la Tisa la Wawakilishi ulioanza tarehe 10 Mei, 2017. Shughuli zote zilizopangwa katika ratiba ya Mkutano huu zimekamilika kwa wakati na kwa ufanisi wa kupigiwa mfano.

Mhe. Spika, namshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuiweka nchi yetu katika hali ya amani, utulivu, umoja na mshikamano mkubwa. Hali ambayo imeendelea kuipa nafasi Serikali na wananchi wote kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na mafanikio. Naendelea kuwasisitiza viongozi pamoja na wananchi wote kwa jumla tuendelee kuidumisha kikamilifu amani na utulivu huo kwani bila ya amani hakuna maendeleo.

Mhe. Spika, kwa umuhimu na uzito wa kipekee nampongeza kwa dhati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa kuisimamia vyema amani katika nchi yetu na kuendelea kutoa maelekezo na miongozo kwa viongozi na watendaji mbali mbali wa serikali katika kuleta ufanisi katika utendaji wetu wa kazi za kuwatumikia wananchi. Tunaamini kwamba, miongozo na maelekezo hayo yanasaidia sana katika kuongeza uweledi na uwajibikaji unaotoa mchango mkubwa wenye kuleta ufanisi katika maendeleo nchini.

Mhe. Spika, pia naomba kuchukua nafasi hii kutoa shukrani kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa namna anavyosimamia utekelezaji wa ahadi zake katika Mikoa, Wilaya na Taasisi za Serikali ikiwemo ahadi ya nyongeza ya mishahara ya watumishi wa umma. Hivi karibuni alipoongeza mishahara ya kima cha chini kwa asilimia mia moja, yaani kutoka shs. 150,000 hadi 300,000/=. Dkt. Ali Mohammed Shein akitoa ahadi anaitekeleza.

Mhe. Spika, vile vile napenda kutoa pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa namna anavyosimamia utekelezaji wa majukumu yake ya kuiongoza nchi yetu. Sote ni mashuhuda wa juhudi zake hizo za kusimamia utendaji na nidhamu kwa wafanyakazi na watumishi wa umma, kupiga vita rushwa na uhujumu wa uchumi, kupambana na madawa ya kulevya, ukwepaji wa kulipa kodi pamoja na kusitisha usafirishaji haramu wa rasilimali za nchi yetu ikiwemo mchanga wa madini ili kuokoa pato la nchi yetu. Ni mategemeo yetu kuwa,

jitihada hizo zitaisaidia sana serikali katika hatua za kudhibiti mapato na kuimairisha uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, pongezi pia zimuendee Kamanda Simon Nyakoro Sirro kwa kuteuliwa kwake kuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi, Tanzania (*IGP*). Uteuzi huo unaonesha imani ya Mhe. Rais aliyonayo kwake kwa utendaji wake wa kazi. Ninaamini kwamba ataendelea kuliimarisha Jeshi la Polisi katika utekelezaji wa majukumu ya ulinzi wa raia na mali zao kwa uadilifu pamoja na kudumisha amani nchini.

Mhe. Spika, natoa pole wa wananchi wote waliopatwa na maafa ya mvua kubwa za masika ambayo imeikumba Mikoa yote ya Zanzibar pamoja na upepo mkali uliotokea katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar ikiwemo Fukuchani Wilaya ya Kaskazini A, Mwanakwerekwe, Kinuni, na Nyarugusu kwa Wilaya ya Magharibi B na Changaweni Wilaya ya Mkoani, Pemba.

Kufuatia maafa hayo, miundombinu kadhaa ikiwemo nyumba zipatazo 150, barabara na madaraja yaliharibika pamoja uharibifu mkubwa wa mazao. Idadi kubwa ya wananchi walikosa makaazi na walipatiwa hifadhi kwa ndugu, jamaa na majirani. Serikali inapenda kuwapongeza wananchi wote kwa kushirikiana na kuonyesha upendo na umoja bila ya kujali itikadi zao za kisiasa. Kitendo hiki cha kiungwana kinastahili kupongezwa na kuendelezwa kwani sote ni wamoja na ni ndugu.

Mhe. Spika, nawapongeza wananchi wakiwemo wafanya biashara, Mashirika ya Serikali, Taasisi Binafsi, Asasi za Kidini na watu binafsi kwa kujitokeza kwa moyo wao wa dhati wa kuwasaidia ndugu zao waliopatwa na maafa hayo.

Mhe. Spika, pia nawashukuru Wajumbe wa Kamati za Kukabiliana na Maafa, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya zote Unguja na Pemba na Kamati zao za Ulinzi na Usalama, Idara Maalum za SMZ, Vyombo vya Ulinzi na Usalama vya Jamhuri ya Muungano, Idara mbali mbali za SMZ, Mabaraza ya Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri, Madiwani na Masheha kwa kazi kubwa walizozifanya wakati wa kukabiliana na maafa hayo. Kwa upande wa serikali tutaendelea kutekeleza wajibu wetu wa kuhakikisha hali na ustawi wa wananchi na miundombinu inarejea katika hali yake ya kawaida.

Mhe. Spika, naomba tufahamu kuwa maafa ni sehemu ya mitihani ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwetu na hatuna budi tuipokee na tumshukuru kama alivyotuelekeza katika Qur-ani Tukufu Suratul Bakara aya ya 155 - 156 zenye tafsiri ifuatayo naomba kunukuu.

> “Tutakujaribuni kwa kukutieni mitihani mbali mbali miongoni mwa khofu, njaa, upungufu wa mali na nafsi na mazao, na wape habari njema wenye kusubiri, ambao wakipatwa na msiba husema hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea”. Mwisho wa kunukuu.

Mhe. Spika, ninawanasihi wananchi tuendelee kuwa na subira, kushirikiana na kusaidiana katika mtihani huu kwa mujibu wa mila, utamaduni silka, tabia na mwenendo wetu wa kila siku.

Mhe. Spika, hivi sasa imekuwa ni desturi kila unapowadia msimu wa mvua nchi yetu hukumbwa na mripuko wa maradhi ya kipindupindu pamoja na matumbo ya kuharisha. Suala hili ni la kusikitisha sana, hasa ikitiliwa maanani kwamba, maradhi ya mripuko ikiwemo kipindupindu husababishwa na vimelea vinavyopatikana katika maji yasiyokuwa safi na salama ambayo huchanganyika na kinyesi.

Mhe. Spika, maeneo mengi yanayokumbwa na maradhi haya ya kipindupindu husababishwa na uchafu ikiwemo baadhi ya watu kutotumia vyoo, kutupa taka taka ovyo ambazo zimechanganyika na *pampers*. Nyumba nyengine kutokuwepo makaro ya kuhifadhia maji machafu hasa ya vyoo na hivyo kutapakaa mitaani. Lakini cha kusikitisha zaidi kipindupindu hutokea katika maeneo hayo hayo kila mwaka na viongozi wanaohusika hukaa kimya bila ya kuchukua hatua stahiki. Hii sio sahihi kwa viongozi, timizeni wajibu wenu.

Mhe. Spika, takwimu kutoka Wizara ya Afya zinaonyesha kwamba kuanzia tarehe 19 Mei, 2017 ambapo mgonjwa wa kwanza alipotambuliwa kuwa na vimelea vya kipindupindu, hadi kufikia tarehe 17 Juni, 2017, jumla ya wagonjwa 218 wameambukizwa maradhi hayo. Maeneo yalioathirika zaidi ni Wilaya ya Magharibi B na Mjini ikiwemo maeneo ya Kinuni, Kwamtipura, Mtoni Kidatu, Welezo, Tomondo, Rahaleo na Chumbuni. Hali hii imeifanya serikali kuchukua hatua za dharura ikiwemo kuzuia uuzwaji wa vyakula ovyo ili kuinusuru jamii na janga hili.

Mhe. Spika, kuhusu migogoro ya ardhi, hii ni moja ya sekta mama ya maendeleo katika nchi yetu au katika nchi zote duniani. Kwa Zanzibar, sekta ya ardhi ni msingi wa Mapinduzi yetu Matukufu. Tangu mwaka 1964 sekta hii imepita hatua tatu muhimu.
Kipindi cha Mapinduzi iliwekwa msingi wa ardhi yote ya Zanzibar ni mali ya umma, chini ya usimamizi wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Hatua ya pili iliwekwa na Sera ya Ardhi ya mwaka 1982, ambapo usimamizi na matumizi ya ardhi uliwekwa na sheria tisa zilizotungwa kwa ajili ya kusimamia masuala ya ardhi.

Awamu ya Saba chini ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein, imeanzisha Awamu ya Tatu na kutengeneza mfumo mpya wa Utawala wa Ardhi kwa kuanzisha tena Kamisheni ya Ardhi kwa lengo la kuondosha migogoro ya ardhi kupitia Mahakama ya Ardhi. Hata hivyo, pamoja na hatua hizo zote bado tunatambua kuwa tatizo la migogoro ya ardhi bado halijapata ufumbuzi na hasa kwa sababu bado watu hawajataka kufuata sheria.

Mhe. Spika, Serikali ya Awamu ya Saba ipo katika hatua za kutayarisha Sera mpya ya ardhi, kuweka usimamizi imara wa ardhi pamoja na upangaji wa matumizi ya ardhi na haitomvumilia mtu yeyote ambaye atasababisha migogoro ya ardhi hata kama ni kiongozi au mwananchi wa kawaida. Hivi sasa serikali imeamua kufuta maeneo yote yaliyochukuliwa na watu na hayajaendelezwa bila ya kujali wenye maeneo hayo, ili yarudi serikalini na kupangwa upya.

Mhe. Spika, naomba nilizungumzie suala la mchanga na hatua ambazo serikali imezichukua kwani baadhi ya wananchi na wafanyabiashara ya mchanga hawakuielewa vyema azma ya serikali. Hatua iliyochukuliwa ilikuwa na lengo la kuweka utaratibu mzuri wa matumizi bora ya rasilimali hii ambayo waheshimwa tunapaswa tuelewe kuwa, kadri tunavyoitumia inaendelea kumalizika. Serikali imeandaa utaratibu ambao kama sote tutaufuata utaweza kuinusuru ardhi yetu ili itufae sisi na vizazi vijavyo.

Mhe. Spika, kwa kufanya hivyo, yamekuwepo malalamiko mengi ya wananchi ya kuchukuliwa maeneo yao. Serikali haina nia ya kuwadhulumu wananchi, hivyo kwa mtu yeyote ambaye mwenye madai awasilishe vielelezo vyake katika taasisi husika na vitafanyiwa kazi kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo. Tumelizungumza suala hili kwa kirefu ndani ya Baraza hili, hivyo ni imani yangu nategeme kuwa suala hili halitarudi tena Barazani hapa kwa sababu naamini kwamba sasa limefahamika vizuri zaidi.

Mhe. Spika, katika uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Afya kumejitokeza malalamiko mbali mbali ya kiutendaji hasa katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja. Baadhi ya malalamiko hayo ni pamoja na baadhi ya madaktari kutotekeleza wajibu wao, uchafu uliokithiri, lugha chafu za watendaji kwa wagonjwa, huduma zinazotolewa kutolingana na fedha ambazo serikali imekuwa ikizigharamia kwa kila mwezi na namna vifaa vya kuchunguzia kufanyiwa hujuma kwa makusudi ili wahusika wawaelekeze wagonjwa kwenda kwenye hospitali ama zao au wanazopewa kamisheni. Kitendo hiki kama ni kweli si cha haki kufanyiwa wagonjwa ambao wengi wao ni masikini.

Mhe. Spika, katika majumuisho ya Wizara hiyo, Mhe. Waziri wa Afya aliyatolea maelezo malalamiko hayo. Aidha, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Mohamed Aboud alitoa Kauli ya Serikali kuhusu kadhia hiyo. Alisema kuwa dhamira ya serikali ni kutoa huduma bora za afya katika nchi yetu. Serikali imejipanga na inaahidi kuyafanyia kazi mapungufu yote yaliyobainishwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili. Na kuanzia sasa haitowavumilia na haitojali jina la mfanyakazi yeyote hata akiwa na sifa gani akifanya uzembe atachukuliwa hatua kali za kinidhamu na hata kumfukuza kazi mara moja.

Mhe. Spika, Serikali inaendelea na hatua zake za kuimarisha michezo nchini. Hivi karibuni Shirikisho la Soka la Afrika (*CAF*) limeridhia na kuipa uanachama wa kudumu Zanzibar, kufuatia Mkutano Mkuu wa *CAF* wa mwaka 2017. Hatua hii itaiwezesha Zanzibar kushiriki mashindano yote yanayoandaliwa na Shirikisho hili la *CAF*. Aidha, Zanzibar itakuwa na uhalali wa kuhudhuria mikutano, kupokea na kusimamia mafunzo mbali mbali yanayohusu soka na kupata fursa ya kupiga kura katika masuala muhimu ya *CAF*.

Mhe. Spika, kufuatia Zanzibar kupata uanachama huo wa kudumu wa *CAF* kunaashiria uwezekano mkubwa pia wa kupata uanachama wa *FIFA* hali ambayo itapelekea vijana wetu kushiriki katika mashindano ya Kimataifa. Tayari hatua za awali za kuomba uanachama wa *FIFA* zimeshaanza. Kazi tuliyonayo sasa ni kuwaandaa vijana wetu kwa

ajili ya kushindana kwenye mashindano ya Kimataifa ya mpira wa miguu, ili kuiletea nchi yetu heshima ile iliyokuwa nayo huko nyuma.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, Mhe. Rashid Ali Juma pamoja na Waziri mwenzake wa Tanzania Bara, Mhe. Dkt. Harrison Mwakiyembe kwa juhudi zao hadi kufika hatua hiyo.

Mhe. Spika, Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini *TASAF* Awamu ya Tatu ni muendelezo wa utekelezaji wa Mipango na Mikakati ya Serikali ya kupunguza umaskini uliokithiri kwa wananchi wetu kwa kuziwezesha kaya masikini sana kuongeza kipato.

Mhe. Spika, kwa upande wa Zanzibar, Mpango huu umeendelea kutekelezwa kwa mafanikio makubwa ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2017 jumla ya shilingi Bilioni Kumi na Nane, Milioni Thamanini na Tisa, Laki Mbili na Ishirini Elfu, Mia Moja na Thalathini na Saba (18,089,220,137.00) zimelipwa kwa Kaya 32,614 za walengwa wa Mpango huo kupitia Ajira za Muda kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kutokana na mafanikio haya makubwa yaliyopatikana, Washirika wa Maendeleo wakiongozwa na ujumbe wa Benki ya Dunia wameridhishwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa Mpango huu Zanzibar. Ni matumaini yetu kwamba, mafanikio haya yataendelea kuwa chachu ya maendeleo na kufikia malengo ya mikakati ya kupunguza umaskini nchini.

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2016/2017, mafanikio makubwa yamepatikana ambapo ukusanyaji wa mapato umefika asilimia 110 ambayo ni sawa na shilingi bilioni 448.2. Kwa upande wa matumizi ya kawaida yamefikia asilimia 100 ya lengo. Mafanikio haya yameiwezesha serikali kutekeleza majukumu yake kwa uhakika kama iliyojipangia. Naamini kwamba bajeti ya mwaka 2017/2018 ambayo tumeipitisha hivi punde na kwa uongozi imara na mahiri wa Mhe. Rais wetu wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohamed Shein tutaitekeleza kwa asilimia mia moja na zaidi.

Mhe. Spika, katika Mkutano huu wa Sita wa Baraza la Tisa tulijadili na kupitisha Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Bajeti ambayo imejadiliwa kwa utaratibu mpya ambapo Bajeti za Kisekta zimejadiliwa mwanzo na tumemalizia na Bajeti Kuu ya Serikali na Sheria ya Fedha. Shughuli ambayo imefanyika kwa ufanisi mkubwa, Waheshimiwa Wajumbe walipata nafasi ya kuzichangia, kuzishauri na hatimae kuzipitisha Bajeti za Wizara zote.

Mhe. Spika, naomba niwathibitishie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu pamoja na wananchi kwa ujumla kwamba, michango na ushauri uliotolewa tumeupokea na utafanyiwa kazi katika utekelezaji wa shughuli za kila siku ili kuleta ufanisi katika sekta zetu zote.

Mhe. Spika, katika kikao hiki jumla ya maswali ya msingi 170 na maswali ya nyongeza 421 yaliulizwa na yalijibiwa kwa umakini, ufasaha na usahihi na mawaziri wote. Maswali yaliyoahidiwa kupatiwa majibu ya maandishi, majibu hayo yaliletwa haraka sana hapa

Barazani. Napenda kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa umahiri wa kujibu maswali hayo.

Mhe. Spika, mkutano huu pia umejadili jumla ya Miswada Mitano (5) na kuipitisha kuwa sheria. Miswada yenyewe ni:-

i. Mswaada wa Sheria ya (Marekebisho) ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya mwaka 2015.
ii. Mswada wa Sheria ya Matumizi. (*Appropriation Bill*).
iii. Mswada wa Sheria ya Fedha (*Finance Bill*).
iv. Mswada wa Sheria ya kuweka masharti bora ya usimamizi wa ushuru wa stempu na mambo mengine Yanayohusiana na Hayo na kufuta Sheria ya Ushuru ya Stempu (*Stamp Duty*) ya mwaka 1996.
v. Mswada wa Sheria ya kuweka vifungu vya uanzishaji wa kodi itakayojulikana kama ushuru wa bidhaa na huduma zinazoingizwa na mambo mengine Yanayohusiana na Hayo, (*Excise Duty*).

Aidha, ilikuwepo miswada iliyosomwa kwa mara ya kwanza ambayo ni:-

1. Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara (*Zanzibar Business Council*).
2. Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 3 ya 1995 na kuanzisha upya Mahakama ya Kadhi na kuweka masharti mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba, kupitishwa kwa Mswaada wa Sheria ya (Marekebisho) ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam.4 ya mwaka 2015, kutaondosha changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa sheria ya awali ambapo tatizo kubwa lilijitokeza katika ujazaji wa fomu ya mali na madeni.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kuwaondoa hofu viongozi na wananchi kwamba, kinachotakiwa katika sheria hii ni uwazi na uwajibikaji hivyo, waendelee kutoa mashirikiano zaidi kwa serikali na taasisi zake katika utekelezaji wa sheria hii. Kwa ujumla miswada yote tuliyoipitisha katika kikao hiki itasaidia katika kuweka misingi bora ya utendaji, uwazi na pia kukuza uchumi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, hali kadhalika, Waheshimiwa Wajumbe wamepokea Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu ya Serikali ya mwaka 2014/2015 ambayo Waheshimiwa Wajumbe watapata nafasi ya kuijadili katika mkutano ujao wa Baraza. Nawaomba Wajumbe waipitie ripoti hiyo kwa makini.

Mhe. Spika, naomba nikumbushe kwamba, Baraza lako Tukufu, lilipokea hoja binafsi ya dharura inayohusu suala la maafa, iliyowasilishwa na Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa), Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Mpendae, ambaye alitaka kufahamu hatua za Serikali zinazochukuliwa katika kujikinga na kupambana na maafa.

Mhe. Spika, serikali ilitoa ufafanuzi wake kwamba, itaendelea na hatua zake za kukabiliana na maafa kupitia Kamati ya Kitaifa ya Kukabiliana na Maafa, ambayo itashirikiana na Kamati za Mikoa, Wilaya, Shehia pamoja na wananchi kwa ujumla katika kukabiliana na maafa pamoja na utoaji wa msaada kwa watakaoathirika na maafa hayo.

Aidha, hoja binafsi nyingine ilitolewa na Mhe. Asha Abdalla Mussa, Mwakilishi wa Jimbo la Kiwengwa. Katika hoja hiyo pia serikali pia ilitoa ufafanuzi wa kina kuhusu jambo hili ambalo limekuwa kero kwa wananchi na serikali pia. Hivyo, hatua madhubuti zitachukuliwa na serikali ili kukomesha vitendo hivyo.

Mhe. Spika, wajumbe pia waliipokea ripoti ya utekelezaji ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar kuhusu utekelezaji kwa kipindi cha Oktoba, 2013 – Disemba, 2016. Wajumbe waliijadili ripoti hiyo na hatimae kuipitisha. Ninawahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kwamba ushauri walioutoa utafanyiwa kazi na serikali.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena napenda kutoa pongezi kwako Mhe. Spika, Mhe. Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza kwa kuliongoza vizuri na kwa ufanisi mkubwa Baraza hili. Hekima na busara zenu zimesaidia sana katika kuumaliza mkutano huu salama na kwa mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Naomba pia kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kutumia nafasi na haki yao ya Kikatiba na Kidemokrasia ya kuihoji na kuisimamia serikali. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri kwa namna walivyojibu maswali kwa kutoa ufafanuzi wa kina na kwa ufasaha.

Mhe. Spika, napenda kuwashukuru wale wote waliotuwezesha kukamilisha shughuli zilizopangwa kwenye Mkutano huu kwa ufanisi mkubwa tukiwa katika hali ya amani, utulivu, upendo na mshikamano mkubwa. Pongezi hizo pia ziwafikie watendaji wote wa Baraza hili la Wawakilishi wakiongozwa na Katibu wa Baraza, Ndugu Raya Issa Msellem. Vile vile, nawapongeza Wakalimani wetu wa lugha ya alama ambao wamewawezesha Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi wenye ulemavu wa kusikia kufuatilia yote yaliyokuwa yakiendelea ndani ya Baraza hili. Halikadhalika, nawashukuru wanahabari kwa kufanya kazi ya kuwahabarisha wananchi wetu yale yaliyokuwa yakiendelea hapa Barazani.

Mhe. Spika, kwa kumalizia niwatakie Waheshimiwa Wawakilishi kila la kheri na mafanikio mema katika kuwatumikia wananchi wao Majimboni mwao. Pia, nachukua nafasi hii kuwataka waumini na wananchi wote kwa jumla waendelee na ukamilishaji wa Funga ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa kufuata maelekezo ya Viongozi wetu wa Dini.

Ninawatakia Waheshimiwa Wajumbe wote na wananchi wote kwa ujumla, Sikukuu njema ya Eid el fitri. Aidha, nawatakia safari njema na ya salama ya kurudi Majimboni mwenu na hasa wale wajumbe wenzetu wanaokwenda Pemba. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kwa heshima na taadhima kutoa hoja kwamba, Baraza lako Tukufu liakhirishwe hadi siku ya Jumatano tarehe 27 Septemba, 2017 saa 3.00 barabara za asubuhi Mwenyezi Mungu akitujaalia uhai na uzima.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa naomba niwahoji wale wote wanaounga mkono hiyo hoja kwamba tuliakhirishe Baraza mpaka tarehe 27 Septemba, 2017 wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaakhirisha naomba nitoe tangazo. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti anawatangazia wajumbe wake waonane ukumbi Nam. 2 mara baada ya kuakhirisha.

Baada ya maelezo hayo sasa napenda niliakhirishe Baraza la Wawakilishi mpaka siku ya Jumatano, tarehe 27 Septemba, 2017 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 5.30 asubuhi Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 27 Septemba, 2017 saa 3.00 asubuhi)

WIMBO WA TAIFA

(Hapa wimbo wa Taifa uliimbwa kuashiria kuakhirishwa kwa Mkutano)